Jumatano Novemba 8, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581488

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com



**KONATE AKIRI ANATAKA KUICHEZEA PSG** UKURASA 22

UKURASA WA 4

**TGNP** yajivunia miaka 30 mabadiliko mifumo ya sheria



UKURASA WA 17

**Mwinyi** azishukuru WB, EU ushirikiano serikali Australia



# Waziri ataja vikwazo utekelezaji wa bajeti

• **Wabunge** wafichua mbinu maofisa serikali wizi mabilioni... *Endelea ukurasa 2*




## Wafanyabiashara Kariakoo hatimaye wataka aliyechoma moto atajwe hadharani

UKURASA 3



# DC aagiza Lema kuhojiwa kwa madai uchochezi, mwenyewe ajibu

UKURASA 3

MICHEZO **ROBERTINHO AACHA TIMUA TIMUA SIMBA** UK.24 **KATUNI** UK.6



Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Dodoma, Fatma Toufiq, akichangia maoni yake kwenye Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri ataja vikwazo vitano utekelezaji bajeti

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ametaja vikwazo vitano vinavyoikabili serikali katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23.

Moja ya vikwazo hivyo, kwa mujibu wa Dk. Nchemba ni ukwepaji kodi kwa njia mbalimbali unaofanywa na wafanyabiashara.

Dk. Nchemba alisema hayo juzi wakati akiwasilisha bungeni Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 ambao unaonyesha kuwa serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 47.4.

Alitaja changamoto zingine kuwa ni kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali zikiwamo petroli, mbolea na chakula kutokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine, kudorora kwa uchumi wa dunia hususani katika masoko ya fedha na mabadiliko ya tabianchi.

"Uwepo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kodi kwa kuingiza bidhaa nchini kupitia njia za udanganyifu ikiwamo magendo, mwitikio mdogo wa kutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki za EFD wakati wa mauzo ni mojawapo ya changamoto tulizokumbana nazo wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2022/23," alisema.

**HATUA ZILIZOCHUKULIWA**

Waziri Nchemba alisema baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya bidhaa za petroli na mbolea ili kupunguza gharama za uzalishaji na kudhibiti mfumuko wa bei.

Alitaja hatua nyingine kuwa ni kuendelea kuboresha sheria za kodi, uwekezaji pamoja na biashara, kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato, kuimarisha doria maeneo ya mipakani, kutoa elimu kwa walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki za EFD.

Waziri Nchemba pia alisema serikali ilianzisha tuzo za uzalendo kupitia mfumo wa risiti za kielektroniki inayotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni na kuendelea kusimamia sera za bajeti na fedha.

**FURSA ZILIZOJITOKEZA**

Kadhalika, Waziri alisema fursa zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti ni pamoja na ongezeko la mahitaji ya chakula katika soko la dunia, kuongezeka kwa soko la ndani kutokana na ongezeko la idadi ya watu.

Alitaja vingine ni uwapo wa nguvukazi kubwa ya taifa ambayo ni




vijana, ukuaji wa miji ambao umekuwa ukifungua fursa nyingi za kiuchumi, ufanisi mdogo katika matumizi ya faida ya jiografia ya nchi kuhudumia nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Alisema pia uwepo wa amani, umoja na utulivu wa uchumi, ongezeko la bei ya vito vya thamani katika soko la dunia, uwepo wa vyumba vichache vya kuhudumia watalii ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watalii na mahitaji ya viwanda vya ndani kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi.

## Wabunge wafichua mbinu maofisa serikali wizi wa mabilioni fedha

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wamefichua baadhi ya maofisa serikali walivyokuwa wakinufaika na wizi wa fedha uliokua unasababishwa na kutokuwapo na mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato katika baadhi ya taasisi na maeneo.

Wamesema licha ya baadhi ya maeneo hivi sasa kuwekwa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji mapato, bado kuna maeneo mengine wananchi wanatumia mfumo wa malipo ya fedha taslimu hali inayosababishia serikali upotevu wa mabilioni ya shilingi.

Walisema hayo jana bungeni wakati wakichangia Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka 2024/25.

Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga, alisema kutokuwapo kwa mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato katika baadhi ya maeneo, kumeisababishia hasara serikali huku akipendekeza uharakishwaji wa kufungwa kwa mfumo huo katika kila taasisi na maeneo nyeti nchini.

Sanga alitolea mfano wa Daraja la Nyerere (Kigambani) mkoani Dar es Salaam kuwa awali ukusanyaji wa mapato ulikuwa Sh. milioni 300 kwa mwezi lakini baada ya kufungwa kwa mfumo wa kielektroniki, makusanyo yalipaa hadi Sh. bilioni 1.3.

Mfano mwingine, Sanga alisema Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Tumbi mkoani Pwani, ilikuwa inakusanya Sh. milioni 12 hadi milioni 13 kwa mwezi kabla ya mfumo, lakini baada ya kufungwa makusanyo yaliongezeka hadi Sh. milioni 400.

"Ukienda Mamkala ya Mapato Tanzania (TRA), hospitalini mifumo iko chini. Baadhi ya watumishi wanatumia mbinu ya kuchezea mifumo ili kuiibia serikali. Mteja ukifika wanakwambia hakuna mtandao au mtandao uko chini. Lakini hata siku moja sijawahi kusikia mfumo wa kulipa mishahara uko chini," alisema.

Sanga alisema ni wakati sasa wa serikali kuhakikisha kila taasisi kunafungwa mfumo wa ukusanyaji mapato wa kielektroniki, kwamba hakuna sababu ya watu kukutana ana kwa ana kwa sababu inatengeneza mianya ya rushwa.

Pia alitolea mfano mwingine wa Kituo cha Mabasi Msamvu mkoani Morogoro ambacho ni mwaka wa tatu sasa viongozi wanavutana kuhusu kufunga mfumo wa kielektroniki huku baadhi wakuitaka makusanyo yaendelee kukusanywa kwa fedha taslimu.

Mbunge wa Singida Maghaibi (CCM), Elibariki Kingu, alisema Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, awali ilikuwa inakusanya Sh. milioni 800 kabla ya kufungwa kwa mfumo wa malipo kwa kielektroniki lakini sasa wanakusanya Sh. bilioni 3.8 kwa mwezi.

Alisema Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) walikuwa wanakusanya Sh. milioni 300 hadi 400 kwa mwezi, lakini baada ya kufungwa kwa mfumo, sasa wanakusanya Sh. bilioni 1.5.

"Watu wanakataa mfumo wa kielektroniki kwa sababu wanataka kuendelea kuiba. Hii mifumo ya ukusanyaji mapato kwa kielektroniki imefungwa na vijana wa Kitanzania. Ni wakati sasa wa Serikali kuhakikisha kila idara, sehemu kufungwe mfumo huu ili kudhibiti upotevu wa makusanyo," alisema Kingu.

Kadhalika, Mbunge wa Madaba (CCM), Dk. Joseph Mhagama, aliishauri serikali kuongeza mauzo nje ya nchi ili kupunguza nakisi ya urari wa biashara.

Pia alishauri kuongezwa kasi ya uuzaji madini nje ya nchi,mazao ya misitu, upanuzi wa huduma za utalii Pamoja na kuuza nyama kwa wingi nje ya nchi.

Naye Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage, aliishauri serikali kuuza malighafi nje ya nchi ili kupata fedha nyingi za kigeni.

HABARI KITAIFA

# Afariki akizibua mtaro kupitisha maji ya mvua

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTU mmoja amefariki dunia baada ya kusombwa na maji ya mvua katika mtaro wa majitaka, Sebleni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Aliyefariki ametajwa kuwa ni Abubakar Abdallah (25), ambaye alifikwa na mauti wakati alipoenda kuzibua mtaro wa maji uliokua umeziba.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Kamisheni ya Maafa, Makame Khatib Makame, alisema mvua imeleta athari kubwa kwa kusababisha familia 1,140 kuathirika baada ya nyumba zao kujaa maji.

Alisema tukio la kufariki kwa kijana huyo lilitokea Novemba 5 na mwili wake ulipatikana Novemba 6 katika eneo la Kinazini, Mjini Unguja.

Mkurugenzi aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa sababu bado mvua kubwa inatarajiwa kunyesha ikiwamo ya El-Nino.

Aliwataka wananchi wanaoshi mabondeni kuhama ili kuepukana na athari.

Wakati mvua ikinyesha, katika baadhi ya nyumba huko eneo la Ziwa Maboga wameonekana samaki aina ya kambare wakielea ndani ya nyumba hizo.

Eneo hilo kipindi cha mvua huathiriwa kwa nyumba kujaa maji.

Mkuu wa Wilaya wa Magharib B, Hamida Mussa, aliwataka wananchi wanaoshi karibu na ziwa hilo kuhama kwa sababu wapo katika hatari kutokana na kufurika kwa maji.

**Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Kamisheni ya Maafa, Makame Khatib Makame, alisema mvua imeleta athari kubwa kwa kusababisha familia 1,140 kuathirika baada ya nyumba zao kujaa maji.**

# DC aagiza Lema kuhojiwa madai ya uchochezi, mwenyewe ajibu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Peter Lijualikali, amemwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya hiyo, kumhoji kiongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Godbless Lema, kwa tuhuma za kutoa kauli ya uchochezi.

Lema anadaiwa kutoa maneno ya uchochezi ya kuhatarisha maisha ya Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Korongwe Forodhani, Daudi Ismail.

Inadaiwa kuwa Oktoba 24, mwaka huu, Lema akiwa kijijini hapo kwenye mkutano wa hadhara, alitoa kauli yenye ukakasi inayosababisha ofisa huyo kuishi kwa hofu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Lijualikali alisema: "Katika mkutano huo, mmoja wa viongozi hao wa CHADEMA anayejulikana kwa jina la Godbless Lema, alisikika na alionekana akitoa kauli za kuchochea mauaji kwa kuhamasisha vikundi vya vijana na wanaume wa chama hicho wakatishe uhai wa Mtendaji wa Kijiji, Daudi Ismail.

"Tunapozungumza hapa muda huu, hali ya usalama katika eneo hilo na uhai wa maisha ya Daudi Ismail, yako shakani. Tangu siku hiyo, kumekuwa na sintofahamu kubwa kutokana na vitisho dhidi ya maisha yake, ambavyo vinaonekana ni kuanza kutekelezwa kwa maelekezo ya kauli hiyo ya Lema aliyowaelekeza viongozi, wanachama na wafuasi wake," alisema.

Alisema kiongozi huyo alitumia vibaya fursa aliyotoa Rais Samia Suluhu Hassan ya kurejesha mikutano ya hadhara, ambayo inapaswa kuwa nafasi ya wao kunadi sera zao, kama wanazo kweli.

"Kauli hizo za kuhamasisha mauaji zilizotolewa na viongozi wa CHADEMA, kwa mara nyingine zimesadifu kabisa hoja ambazo zimekuwa zikielekezwa kwao kuwa chama hicho kinafuga vikundi vya kufanya vitendo vya utekaji na mauaji, kama ambavyo aliyewahi kuwa kiongozi wao wa juu kabisa, amekuwa akinukuliwa akisema kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii," alisema.

"Kutokana na hali hiyo, OCD wa Nkasi namwagiza kuchukua hatua za kisheria mara moja, kufanya upelelezi dhidi ya uchochezi wa mauaji aliofanya Lema na kuhatarisha uhai na maisha ya watu na hali ya usalama katika eneo letu, hali ambayo inakwaza juhudi za wananchi katika kujishughulisha na shughuli za maendeleo," alisisitiza.

Nipashe ilimtafuta Ofisa Mtendaji huyo kuzungumzia tukio hilo na kusema matamshi aliyotoa kiongozi huyo yamesababisha kufanya kazi kwenye mazingira magumu kutokana na eneo lake kuwa ni mwambao wa Ziwa Tanganyika ambako kuna mwingiliano wa watu wengi na uvuvi haramu.

Hata hivyo, Nipashe ilipomtafuta Lema, alikataa kutoa kauli ya kuua na kudai kuwa alitamka neno la kisiasa 'muoeni'.

Lema alisema: "Siwezi kutamka neno kama hilo. Nimesema muoeni, yaani fungeni naye ndoa. Ni neno tu la kisiasa nilikuwa namaanisha mdhibitini."



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dar es Salaam (DAWASA), wakiunganisha mtandao wa majisafi kwenye bomba la inchi 3 kutoka kwenye bomba la inchi 4 kwa umbali wa mita 800 katika eneo la njia panda, Tegeta A, kwa lengo la kusogeza huduma kwa wakazi wa maeneo hayo, mkoani humo jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**.

# Wafanyabiashara Kariakoo wataka aliyesababisha moto atajwe

**Na Maulid Mmbaga**

WAFANYABIASHARA wa Kariakoo waliounguliwa na bidhaa zao siku chache zilizopita, wametoa rai kwa uongozi wa mkoa wa Dar es Salaam na serikali kuu kumtaja aliyesababisha ajali hiyo ya moto ili sheria ichukue mkondo wake na wapate stahiki zao.

Kwa mujibu wa wafanyabiashara hao, ambao ni wauzaji wa vipuri vya magari, taarifa ya uchunguzi wa awali uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, ilibainisha kuwa moto huo ulioteketeza maduka yao, haukuwa ajali bali ni hujuma iliyofanywa na mtu kama ilivyoonyeshwa kupitia kamera za ulinzi (CCTV).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, mmoja wa waathirika wa janga hilo, Moshi Mahita, alisema tangu waunguliwe na bidhaa zao ni zaidi ya mwezi sasa lakini hawaoni chochote kikifanyika licha ya taarifa ya uchunguzi kutolewa. Alisema jambo hilo linawaumiza kwa kuwa wanahisi kuna mtu anawafanyia hujuma.

"Leo (jana) ni siku ya 38 watu wanapata shida. Wenzetu wamepata fursa ya kwenda kurepea majumba yao sisi tunaambiwa mpaka kibali ambacho ni wiki mbili sasa tunapambana hatujakipata. Kosa letu ni nini hatuambiwi ni wapi tunakosea?"

"Wakati mwingine tunajitoa wenyewe kwenda kwenye wizara, wilaya na mkoani kuuliza kuna nini. Sisi tunapata shaka, tunaamini sauti zetu hazifiki mahali husika kutokana na hawa wanaotuzunguka hapo kati. Kuna watu wanatuziba midomo kwa njia zao wanazozijua," alisema Mahita.

Pia alisema kila wanayemuuliza hawampi jibu linaloeleweka akisema viongozi wao hawawatendei haki kwa kile alichosema jua na mvua vinawaishia lakini hawatakiwi kuweka hata turubai kwa ajili ya kujikinga na jua.

"Mimi imani yangu inanituma yuko mtu hapa anaona bora iwe hivi labda analengo lake. Tunawaomba wadau watusaidie kupaza sauti zetu zimfikie Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Katibu Muenezi wa CCM, Paul Makonda. Naamini mmeliona na mnalisikia hili," alisema Mahita.

Alisema wanaunga mkono kwamba tukio hilo ni hujuma licha ya kuonyesha kushangazwa kwamba ni kwa nini mpaka sasa mhusika habainishwi na hawapati majibu kila wanapohoji.

Kondo Ramadhani, ambaye pia ni mfanyabiashara katika eneo hilo, alisema tangu tatizo hilo litokee, hakuna chochote wanachokiona kikiendelea zaidi ya kusulubika na njaa na kwamba ilifika mahali walizuiwa kuingia katika eneo hilo lakini walivunja mlango na kuingia.

"Tunamwomba mkuu wa mkoa kuchukua hatua kali kwa wale waliohusika na hujuma hii, mkono wa sheria uchukue mkondo wake bila kujali nani ametuchomea moto na kutuathiri kiasi hiki. Pia tunamwomba ajue sisi tunaathirika hapa na tunatii mamlaka ndiyo maana tuko kimya.

"Asichukue muda mrefu kuchukua hatua za kisheria kwa wale waliohusika na hujuma hii ambao yeye anawajua na amewaona kupitia kamera ya CCTV. Tunamthibitishia kuwa eneo hili ni letu na yeyote mwenye mashaka aende ardhi," alisema Ramadhani.

Siku chache zilizopita, Chalamila aliwaelekeza wafanyabiashara hao kutofanya shughuli yoyote katika eneo hilo hadi taratibu za uchunguzi zitakapokamilika.



Vibanda vya kisasa kwa ajili ya wafanyabiashara wa mitumba, vinavyojengwa na Manispaa ya Ubungo katika soko la Mawasiliano (Simu 2000), Sinza, Dar es Salaam, vikionekana kwenye hatua za kukamilika jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TGNP yajivunia miaka 30 mabadiliko mifumo ya sheria

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Kijinsia Tanzania (TGNP), unasherehekea miaka 30 tangu kuanzishwa, ikijivunia mabadiliko makubwa katika taifa kwenye mifumo ya sheria inayohalalisha matendo ya kibaguzi.

Maadhumisho hayo yamewaleta pamoja zaidi ya watu 2,000 kutoka nchi 14 duniani Tanzania ikiwamo, ambayo mgeni wa heshima ni Mkurugenzi Mtendaji wa UN Women duniani na Makamu wa Rais wa Afrika Kusini, akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo, Dk. Phumuzike Mlambo-Ngcuka.

Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gemma Akilimali, alisema kwa kipindi chote juhudi za pamoja za taasisi za masuala ya kutetea haki, walifanya kazi kwa pamoja na kuchangia kwa kiasi kikubwa kubadilishwa miundo ya sheria ambayo awali ilikuwa ikihalalisha ukiukwaji na kuwa kikwazo kwa haki za wanawake.

Alizitaja baadhi ya sheria hizo kuwa ni ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA) mwaka 1998, Sheria za Vijiji na Ardhi namba 4 & 5 za mwaka 1999, Sheria ya Mtoto sura ya 13 (2009) na kanuni zake.

Mabadiliko mengine ni kuwapo miongozo ya uzingatiwaji wa masuala ya kijinsia katika bajeti na mikakati ya serikali na uundwaji wa madawati ya kijinsia katika taasisi za umma, uundwaji wa madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi, uwapo wa vituo vya mkono kwa mkono (one stop centres) kwa ajili ya kurahisisha mashauri ya ukatili wa kijinsia.

Mengine ni ushiriki katika muungano wa wanawake watetezi kuhusu katiba, uchaguzi na uongozi, ulioanzishwa kwa lengo la kusaidia kupatikana kwa Katiba mpya.

Kwa mujibu wa Akilimali, muungano huo ulifanikiwa kuingiza masuala 11 kati ya 12 yaliyopendekezwa katika Katiba ambayo kwa bahati mbaya mchakato wake uliishia njiani.

"TGNP imekuwa mojawapo ya taasisi zilizofanya chambuzi za kina za kifeminia dhidi ya mifumo kandamizi ukiwamo mfumo dume, uliberali mamboleo, ubaguzi wa kirika, kijinsi na kijiografia. Chambuzi hizo zimekuwa zikitumika katika mijadala ya kitaifa ambayo imekuwa chachu ya kuleta mabadiliko na fikra mbadala," alisema.

Mwenyekiti alisema utafiti na uchambuzi wa kifeminia umeonesha wazi athari za mifumo kandamizi na miundo ya uchumi wa kibepari na uliberali mamboleo kwa watu maskini hususani wanawake.

"Mijadala tuliyoijenga ilichangia katika mabadiliko kadhaa ya kisera ikiwamo kuingiza suala la matumizi ya muda katika shughuli za huduma au zisizo na malipo (time use and unpaid care work) katika tafiti za kitaifa," alisema.

Akifungua maadhimisho hayo mgeni wa heshima, Mlambo-Ngcuka, aliwapongeza wanaharakati wa Tanzania kwa uelewa wao wa kina kuhusu ugumu wa harakati za kupigania usawa wa kijinsia, harakati ambazo zinahusisha mwingiliano wa vizazi mbalimbali, haki za watu wenye ulemavu, watu wa rangi zote na watu wenye mitazamo huru ya kijinsi.

"Ufeministi wa kimageuzi unaitaka jamii kuhakikisha kuwa haki za watu zinalindwa na kuheshimiwa. Unalenga kupinga na kubomoa mifumo ya kimfumo dume yenye mizizi mirefu katika jamii. Usawa wa kijinsia umekuwa ukitazamwa kwa misingi ya kimfumo dume," alisema.

Aidha, alisema athari mbaya za mtazamo huo huwakumba wanaume na wanawake na kwamba makundi hayo ambayo ni wanufaika wa mfumodume wanapaswa kushirikishwa kikamilifu katika mapambano hayo.

"Nchini Tanzania na barani Afrika kwa ujumla, tunapaswa kushughulikia suala la usawa wa kijinsia kwa mkabala jumuishi. Tunapaswa kukabiliana na vitendo vya ukatili dhidi ya mtoto wa kiume huku tukishughulikia masuala muhimu yanayomhusu mtoto wa kike," alisema.

Spika mstaafu, Anne Makinda akizungumza kwenye maadhimisho hayo, alisema kazi kubwa imefanywa na TGNP kwa kujenga uelewa na wadau wengine ikiwamo serikali, AZAKI, wanazuoni na vyombo vya habari, wadau wa maendeleo.

"Tunapoona masuala ya usawa wa jinsia yameingizwa kwenye sera, mipango na bajeti, TGNP imechangia kwa kiasi kikubwa. Tunapozungumzia bajeti yenye mtizamo wa jinsia, TGNP ndiye kinara na mwanzilishi wa dhana hiyo katika nchi yetu ya Tanzania na katika Bara la Afrika," alisema.

"Nimekuwa serikalini muda mrefu na nilianza kushika nafasi ya ubunge, nikashika nafasi ya uwaziri ambapo nilipata nafasi nzuri ya kufanya kazi kwa karibu sana na TGNP pamoja na asasi nyingine za kutetea haki za wanawake na watoto.

"Vile vile, wakati nasimamia Bunge kama Spika wa Bunge wa kwanza mwanamke ambaye niliongoza Bunge kipindi ambacho kulikuwa na vijana wengi na wabunge wengi kutoka vyama vya upinzani niliweza kushirikiana na TGNP na asasi nyingine za kutetea haki za wanawake kusongesha mbele ajenda ya usawa wa jinsia Tanzania," alisema.

# Serikali kuzuia dawa nne kutoka nje

**Na Beatrice Shayo**

MFAMASIA Mkuu wa Serikali, Daud Msasi, amesema serikali ina mkakati wa kuzuia dawa nane ambazo zinaingizwa nchini na badala yake zitakuwa zinanunuliwa kutoka kwa wazalishaji wa ndani.

Pia imesema asilimia 80 ya mahitaji ya dawa, vifaa na vifaa tiba vinaagizwa kutoka nje ambavyo gharama yake ni zaidi ya Sh. bilioni 300 na kwamba mkakati wa serikali sasa ni kuhakikisha fedha hizo zinatumiwa na wazalishaji wa ndani.

Msasi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kikao maalum ambacho kimeandaliwa na Bohari ya Dawa (MSD) kwa ajili ya kujadiliana na kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa za afya zikiwamo dawa, vifaa na vifa tiba nchini ili kupunguza utegemezi unaoendelea sasa.

Alisema zaidi ya asilimia 80 ya mahitaji ya dawa, vifaa na vifaa tiba vinaagizwa kutoka nje ya nchi na kwa lengo la serikali ni kuhakikisha uagizaji huo unapungua kutoka asilimia 80 hadi chini ya asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

Juhudi mojawapo, alisema ni kukakaa na waagizaji wa ndani ili kuangalia changamoto ambazo wanakutana nazo na maeneo ambayo wanapendekeza kwa ajili ya kuboresha ili serikali kufanyia kazi.

"Dhamira ya serikali ni kuhakikisha jambo hili la uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya nchini linafanikiwa na tayari vipo viwanda vinawekeza tunavyoongeza. Kwa sasa tuna baadhi ya bidhaa yakiwamo maji tiba tumezuia MSD isinunue kutoka nje ya nchi badala yake wanunue katika viwanda ambavyo tayari vipo nchini na vinazalisha kwa kiwango cha kutosha," alisema.

Pia alisema serikali imetoa maelekezo kwa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) kufanya uchambuzi wa bidhaa zinazozalishwa nchini katika zaidi ya viwanda 12.

Alisema lengo ni kuona viwanda hivyo vinakidhi wingi wa uzalishaji na ubora ili litolewe tamko la kuzuia MSD kuagiza nje ya nchi na kutumia wazalishaji wa ndani ili kuhakikisha wanapata soko la bidhaa zao, kukua na kuingia katika ushindani.

Viwanda hivyo, alisema vimekuwa vikizalisha dawa za aina nane na tayari TMDA imeagizwa kuzifanyia uchunguzi kama vinakidhi viwango vya kimataifa, kiasi cha uzalishaji, ubora na baada ya hapo watatoa maelekezo ili kuhakikisha bidhaa hizo zinanunuliwa nchini.

"Serikali tunafahamu kuwa vita hii si ndogo ni kubwa kwa sababu uzalishaji ndani ya nchi maana yake unampunguzie mtu ambaye alikuwa analeta masoko. Tunaendelea kuzitatua hizo changamoto kuhakikisha tunatoa maelekezo ambayo itawawezesha wazalishaji wa ndani kupata soko ndani ya nchi na nje ya nchi," alisema.

Aidha, alisema hivi karibuni serikali imeridhia mkataba wa African Medicines Agency (AMA) ambayo lengo lake ni kulinda bidhaa zinazoingia Afrika na viwanda vya ndani vitasajili dawa na kuuza Afrika.

Mfamasia Mkuu alisema mkutano huo utasaidia kuibua changamoto mbalimbali ambazo serikali itazifanyia kazi kwa lengo la kuboresha na kuhakikisha uzalishaji wa ndani unakuwa na uagizaji kutoka nje ya nchi unapungua ili kufikia mkakati uliopangwa wa mwaka 2030.

"Changamoto ambayo tunaenda kuifanyia kazi baada ya kuanza kuzalisha bidhaa nchini na kueleza hatutaagiza maji tiba nje ya nchi. Tulivyokuwa tunaagiza maji tiba nje ya nchi chupa moja tulikuwa tunanunua kwa Sh. 700 na wazalishaji wa ndani kwa mazingira yaliyopo wanauza kwa gharama hiyo tukianza kununua kwa Sh. 700 kwa mzalishaji wa ndani, tayari mzalishaji wa nje ameishusha hadi Sh. 500 inatupa changamoto uchague wapi pa kwenda," alisema.

Dhamira ya serikali, alisema ni kuhakikisha licha ya changamoto hizo mkakati wao ni kuwalinda wazalishaji wa ndani kuendelea kuwekeza na kukua kiuchumi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa bohari hiyo, Leopold Shayo, alisema bajeti ya MSD kwa ununuzi wa bidhaa za afya nchini ni Sh. bilioni 590 kwa mwaka na asilimia 80 ambayo ni zaidi ya Sh. bilioni 300 zinatumika nje ya nchi.

Alisema kiasi kidogo cha upungufu ya Sh. bilioni 100 zinabaki nchini na zaidi ya Sh. bilioni 300 zingetumiwa na wazalishaji wa ndani badala ya kuzipeleka nje ya nchi.

"Ni eneo ambalo kama wazalishaji wa ndani ni lazima kuangalia ni kwa namna gani wanaweza kufanikiwa katika hili wenzetu China wameweza na nchi nyingine na wameona kuna fursa," alisema.

HABARI KITAIFA

## Serikali yaita wenye changamoto kodi majengo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kama kuna mmiliki wa majengo ambaye ana kero za ulipaji kodi kupitia ununuzi wa umeme, atoe taarifa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili maboresho yafanyike.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Nyamagana (CCM), Stanslaus Mabula, ambaye alitaka kujua mpango wa serikali wa kutenganisha malipo ya majengo kwa nyumba yenye zaidi ya mita moja ya umeme.

Akijibu swali hilo, alisema serikali imeendelea kuboresha ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo wa LUKU kwa nyumba ambayo ina zaidi ya mita moja kwa kuhakikisha inalipiwa moja pekee.

Pia alisema pale inapobainika majengo mawili au zaidi kutumia mita moja tumekuwa tukifanya maboresho ya utozaji kwa kutoza kiasi kinachopaswa kutozwa kwa kila jengo kwa mita iliyopo.

Alisema lengo la hatua hiyo ni kuhakikisha msingi wa utozaji wa kodi ya majengo unazingatiwa na kutokana na wamiliki wa majengo wachache kujitokeza kusajili na kutoa taarifa sahihi za majengo yao, TRA iliendelea na uhakiki kwa kutumia vyanzo kutoka mamlaka mbalimbali za serikali.

Dk. Nchemba alisema kwa sasa TRA inaendelea na maboresho ya taarifa za wamiliki wa majengo.

"Nitumie bunge lako tukufu kwa kuwataka wamiliki wote wa majengo ambao watakuwa na changamoto za ulipaji kodi ya majengo kupitia ununuzi wa umeme ikiwa ni pamoja na uwepo wa mita zaidi ya moja katika jengo, kufika katika ofisi ya TRA iliyokaribu kwa ajili ya kufanya maboresho ya taarifa zao," alisema.

**Dk. Nchemba alisema kwa sasa TRA inaendelea na maboresho ya taarifa za wamiliki wa majengo.**

# TLS yajitosa kumsaidia mjane aliyehukumiwa miaka 22 jela

**Na Francis Godwin,** IRINGA

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), tawi la Iringa, kimeanza mchakato wa kumsaidia mjane Mariam Ngoda (22), mwenye watoto wanne aliyehukumiwa miaka 22 jela kwa kukutwa na vipande 12 vya nyama ya swala.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Iringa.

Mwenyekiti wa TLS Kanda ya Iringa, Wakili Moses Ambindwile na Wakili Cosmas Kishamawe, walisema kwa kushirikiana na mawakili wengine wa mkoani humo wameanzisha mchakato wa kumsaidia mjane huyo ikiwamo kukata rufani.

Aidha, walisema mchakato wa kukata rufani dhidi ya hukumu ya Mahakama ya Mkoa wa Iringa umeanza rasmi na kwamba tangu juzi asubuhi waliendelea na jambo hilo kwa lengo la kumsaidia mwanamke huyo na wengine kupata ushauri na msaada wa kisheria.

Wakili Ambindwile alisema tangu waanzishe mpango wa kutoa msaada na ushauri na msaada wa kisheria, mapokeo ya makundi mbalimbali kwenye jamii ni makubwa na yanafanyiwa kazi kumekuwa na idadi kubwa ya watu wenye kuhitaji msaada huo.

Hukumu hiyo ilitolewa Novemba 3, mwaka huu na Hakimu Mkazi Mkuu Mkoa wa Iringa, Said Mkasiwa baada ya kujiridhisha kuwa mjane huyo mwenye watoto wanne alikutwa na ndoo iliyokuwa na nyama hiyo yenye thamani ya Sh. 900,000 kinyume na sheria.

Akitoa hukumu hiyo kwa mjane huyo mkazi wa Zizi la Ng'ombe mjini Iringa, Hakimu Mkazi Mkoa wa Iringa, Mkasiwa alisema kosa hilo ni kinyume na kifungu cha 86 (1) (2) (c) cha sheria ya uhifadhi wa wanyamapori namba tano ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na kifungu cha 59 (a) (b) cha mabadiliko ya sheria ya mwaka 2016.

Wakati akijitetea bila usaidizi wa wakili, mjane huyo alikiri kukutwa na ndoo yenye nyama hiyo ambayo alidai alikabidhiwa na mtu aliyemtambua kwa jina moja la Fute bila kujua ni nyama ya nini.

Alidai kuwa alilazimishwa kubeba ndoo hiyo na kufikishwa kituoni na kufunguliwa kesi ya kukutwa na nyara za serikali na kosa la uhujumu uchumi.

Hukumu hiyo imezua mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii na maeneo mbalimbali kuhusu adhabu ya kifungo kilichotolewa kwa mjane huyo.

Baadhi ya mijadala iliyotawala ni watu kuhoji wanaoiba mabilioni ya serikali wanaachwa bila kufungwa, lakini wanyonge ndio hupatwa na mkono wa sheria.

"Haki ya Mungu dunia haipo fair (sawa) aliyekamatwa na nyama kwa njaa tu miaka 22 kwa vipande 22 vya nyama.

Aliyefanya ubadhirifu wa bilioni 71 atoe faini ya milioni 12," alilalamika mmoja wa watoa hoja.

Mwingine alisema: "Yaani waiba kuku kwa njaa na kama huyo mama ndio wanafungwa kwa kuwa ni wanyonge maana hizo pesa tu hana za faini."



Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara (kushoto), akipata maelezo kuhusu bandari kavu ya Kwala kutoka kwa Meneja wa bandari hiyo, Alexander Ndibalema (kulia), alipofanya ziara bandarini hapo, Kibaha mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. **PICHA: RESTUTA JAMES**

# TRA yaja na mkakati mpya kwa walipakodi

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeunda idara itakayohudumia walipakodi wa kati 1,680 wakiwamo watu binafsi 40, kampuni, taasisi za serikali na zisizo za serikali.

Katika idara hiyo, kila mfanyabiashara atapewa ofisa mahsusi wa TRA kwa ajili ya kumsikiliza na kufuatilia masuala yake ya kikodi.

Akizindua idara hiyo jijini Dar es Salaam juzi, Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata, alisema idara hiyo inalenga kuboresha huduma kwa walipakodi hao ili kurahisisha makusanyo.

"Sifa za mfanyabiashara kuwa kwenye kitengo cha mlipakodi wa kati ni mauzo ghafi kuanzia Sh. milioni 250 hadi Sh. bilioni 2.5 kwa mwaka...TRA imedhamiria kuboresha huduma kwa walipakodi na kuwaondolea usumbufu," alisema.

Alisema maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, kwa mamlaka hiyo ni kutofunga biashara au kudai kodi kwa nguvu na ili kutekeleza agizo hilo, TRA imeboresha na kurahisisha mifumo ya ulipaji kodi na ritani ili kuchochea ulipaji kodi kwa hiari.

"Ahadi yangu kwenu ni kuwa muundo huu mpya utawasogeza karibu zaidi na huduma bora kwani kila mlipakodi atapewa ofisa mahsusi kwa ajili ya kusikiliza na kufuatilia masuala yake ya kikodi," alisema Kidata.

"Tunaamini utoaji wa huduma bora utamwezesha mlipakodi kutimiza wajibu wake wa kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati."

Alitoa wito kwa wafanyabiashara kuendelea kutoa risiti halali za kielektroniki kila wanapouza au kutoa huduma ili serikali ipate fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo na kupeleka huduma muhimu za kijamii kwa wananchi.

Kamishna wa kodi za ndani, Alfred Mregi, alisema idara hiyo itawahudumia kwa wakati na haraka kundi hilo la walipakodi kwa kupokea na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

Awali, Naibu Kamishna wa idara hiyo, Alex Katundu, alisema lengo la kuanzisha idara hiyo ni kuboresha huduma na kuongeza idadi ya walipakodi hao ili kukuza mapato ya serikali.

Alisema miongoni mwa walipakodi wa kati, zipo kampuni 45 za kidijitali zisizo na ofisi hapa nchini zikiwamo Google na Instagram.

Alitaja baadhi ya mikoa yenye walipakodi wengi wa kati kubwa ni Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Arusha na Mbeya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Adha ya usafiri kwa wananchi Dar ipatiwe ufumbuzi haraka

**KATIKA** jiji la Dar es Salaam kuna ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi inayoendelea katika maeneo mbalimbali, ikiwamo ya usafiri wa mwendokasi kutoka katikati ya mji kwenda Mbagala na Gongo la Mboto. Sambamba na hilo, kuna ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) katika baadhi ya maeneo kwa ajili ya umaliziaji.

Mbali na shughuli hiyo, kuna ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwenye mitaa na sehemu mbalimbali unaoendelea. Lengo ni kuhakikisha maeneo mengi yanapitika kwa urahisi sambamba na kuwapunguzia adha wananchi kukaa muda mrefu barabarani wakati wa kwenda kwenye shughuli zao za kila siku na kurejea nyumbani baada ya kazi.

Pamoja na kazi hiyo kuendelea, kumekuwa na tatizo la usafiri katika baadhi ya maeneo ya miradi. Katika njia ya TAZARA hadi Gongo la Mboto, kwa mfano, imeshuhudiwa wananchi waishio maeneo hayo, wakilalamikia kukosekana kwa usafiri wa mabasi kutokana na barabara kubomolewa ili kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi.

Hatua hiyo imesababisha kuwapo kwa usafiri wa treni pekee, hivyo kufanya wananchi wengi kukosa usafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine. Aidha, kutokana na ukosefu wa usafiri, baadhi ya wananchi wameamua liwalo na liwe, kwa kuning'inia kwenye mabehewa ya treni za Shirika la Reli Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA).

Picha mbalimbali zilionyesha jana na juzi wananchi hao wakiwa wamening'inia kwenye mabehewa huku wengine wakikaa katika chumba cha dereva na wengine kwenye kichwa cha treni. Hali hiyo inaonyesha ni hatari wananchi hao wanaweza kukumbwa na madhara vikiwamo vifo iwapo jambo lolote litatokea.

Kwa ujumla, hali hiyo ni ya kusikitisha na si ya kuichukulia kwa uzito mwepesi kwa kuwa pindi madhara yatakapotokea kuna uwezekano mkubwa wa kushuhudia maafa ambayo hayakutarajiwa.

Ujenzi wa miundombinu ya usafiri wa mwendokasi si jambo geni kwa Tanzania kwani ulianza mwanzoni mwa miaka ya 2010 na kuna mambo ya kujifunza hasa wakati wa ujenzi wa barabara za kutoka Kimara hadi Gerezani, Kivukoni na Kinondoni Morocco.


Wakati wa ujenzi wa njia njia hizo, mkandarasi alibomoa barabara yote kutoka mwanzo hadi mwisho hali iliyosababisha adha kubwa ya usafiri katika maeneo hayo. Pia hali hiyo ilishuhudiwa wakati wa kuanza ujenzi wa Stesheni hadi Mbagala kutokana na mkandaraasi kufanya kama ilivyokuwa kwenye maeneo mengine yaliyotangulia.

Ni wazi kwamba tatizo hilo lilionekana na kwa matarajiio makubwa, ilitarajiwa mamlaka za serikali kwa kushirikisha viongozi wa wizara, mikoa na wilaya pamoja na madiwani wangechukua tahadhari wakati wa kuanza kwa njia mpya ya Gongo la Mboto ili yaliyojitokeza awali yasijirudie. Matokeo yake, wananchi wengi wa gongo la mboto na maeneo ya jirani hivi sasa wanapata adha kubwa kutokana na mambo kama hayo kujirudia.


Ni wakati mwafaka hatua za hadhari zikachukuliwa kabla mambo hayajaharibika zaidi kama ilivyolalamikiwa na baadhi ya wananchi kukaa vituoni muda mrefu bila kupata usafiri na pia kutumia muda mwingi tena kati ya saa mbili hadi nne wakiwa barabarani kutokana na msongamano uliosababishwa na ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi.

Kwa ushauri, hatua inayoweza kuchukuliwa kuepusha tatizo hilo na yajayo ni kwa serikali kukaa na mkandarasi akionyesha mpango kazi wake, hivyo kubomoa kipande husika kwa ujenzi kwa wakati husika badala ya kubomoa barabara mwanzo hadi mwisho na matokeo yake kusababisha wananchi kusumbuka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Jamii bila lishe bora hakuna taifa imara

**ZIPO** sababu nyingi zinazozifanya familia nyingi kushindwa kuzingatia mlo kamili wakati mwingine ni kutokana na umaskini unaosababishwa na ugumu wa maisha, watu wengi wakishindia mlo mmoja hasa vitafunwa.

Kipato kidogo husababisha watu kushindia mahindi ya kuchoma au ya kuchemsha, ugali na kachumbari hata na chumvi, wakiamini kuwa bora mkono umekwenda kinywani.

Wanadhani kuwa ni bora kula chochote iwe ni vitumbua vichache, uji, ukoko na mabaki ya chakula bila kuelewa kuwa kuna maradhi pamoja na hali ya udumavu na utapiamlo yatokanayo na ukosefu wa lishe bora.

Licha ya umaskini na kula mlo duni tena mara moja, ukweli ni kwamba kuna pengo la elimu na kwamba watu hawazifahamu athari za kukosa chakula bora.

> **Licha ya umaskini na kula mlo duni tena mara moja, ukweli ni kwamba kuna pengo la elimu na kwamba watu hawazifahamu athari za kukosa chakula bora.**

Watu wengi hawajafahamishwa athari za kula vyakula vya aina moja mfano wanga zaidi, wengi wanapopenda kula ugali au wali na pengine ndizi kila watu.

Matatizo hayo yatokanayo na ukosefu wa chakula pamoja na kutumia lishe duni yana waathiri zaidi watoto wadogo, wajawazito, wagonjwa na wazee.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), hali duni kilishe inahusisha upungufu, viwango vya ziada au ukosefu wa usawa wa virutubisho katika mwili. Matatizo na maradhi yanayotokana na hali hiyo huwapata watoto wadogo, takribani milioni 41 walio chini ya umri wa miaka mitano duniani kote, shirika hilo linaongeza.

Linafafanua kuwa mathalani watoto wengi wana tatizo la uzito uliopitiliza ambalo nalo ni sehemu ya athari za ukosefu wa lishe bora. Ni kwa sababu wamekuwa na viwango vya ziada vya virutubisho.

Aidha, linasema wengine milioni 159 wanaathirika kutokana na utapiamlo na kwa mujibu wa BBC Swahili, watoto wengi wana ukosefu walishe bora nchini.

BBC inaendelea kusema kuwa licha ya huduma na jitihada za serikali bado shida hiyo inaendelea kujikita na kwenye wodi za watoto kuna watoto wenye ukosefu wa lishe bora.

Ni wakati wa kusisitiza umuhimu wa jamii kuzingatia vyakula bora na mchanganyiko kwa kuwafundisha wanafunzi, wazazi, walezi, wajawazito na hata wanaokwenda hospitalini namna bora ya kuandaa vyakula siyo lazima kuwa na utajiri au fedha nyingi ili kula chakula bora.

Jamii zifahamu kuwa chakula bora ni kile ulichonacho la muhimu ni kufahamu namna bora ya kukipangilia kwa mfano kama nyumbani kuna mahindi, maharage, mboga, maziwa, kuku, mayai na matunda familia zikielekezwa zinaweza kujiandalia mlo bora.

Gharama za vyakula kama vile maziwa, mboga, samaki na nyama zinaweza kuwa kikwazo kwa watu wengine hasa wakazi wa mijini.

Ni dhahiri kuwa kama, wakielekezwa watapewa mbadala mfano badala ya samaki na maziwa wanaweza kutumia maharage, kunde, choroko, njugumawe na mbaazi.

Mahindi au unga ambayo familia nyingi zinayoyaweza pia kuwa lishe bora kwa kuacha kutumia sembe badala yake watumie dona na ikiwezekana kula mahindi ya njano.

Pamoja na hilo ni lazima pia kuwa na maelekezo ya vyakula bora kwa kinamama hasa wanapokwenda kliniki na kwenye huduma za matibabu.

Aidha, familia ziachane na kulisha watoto wao vyakula vya aina moja mfano chips na mayai, vyakula vya kukaanga kama mihogo ambavyo navyo haviwasaidii badala yake huwaongezea uzito na maradhi yakiwamo ya moyo.

Ni vyema pia serikali za vijiji na ofisi za ustawi wa jamii zitazame kaya zenye wahitaji au maskini na kuwapatia msaada ili waweze kupata mlo kamili kusaidia watoto wao. Pamoja na juhudi hizo Wizara ya Afya ianzishe vikundi na vituo mbalimbali vya kutoa elimu ya mlo kamili na faida zake ili Tanzania iwe na watoto wenye lishe bora na kuepukana na udumavu.

HABARI KITAIFA



Wananchi wakipokea vifaa tiba kutoka MSD kwa ajili ya Halmashauri ya Ifakara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MSD yakabidhi vifaa tiba vya mil. 900/- Ifakara

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Bohari ya Dawa (MSD), imekabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 900 kwa Halmashauri ya Ifakara Mji.

Akizungumza juzi, Mbunge wa Kilombero, Abubakar Asenga, alisema ujio wa vifaa hivyo, utasaidia kuboresha huduma za afya na kuishukuru serikali kwa hatua kubwa ya maboresho katika sekta hiyo.

Alisema, jimbo hilo lilikuwa na kero saba muhimu na kubwa ambazo hazijawahi kutatuliwa tangu kupata Uhuru, lakini Rais Dk. Samia amezitatua ikiwamo mradi wa ujenzi wa barabara, maji, ukarabati kituo cha umeme Kidatu, ujenzi wa shule za kata, vituo vya afya, zahanati na hospitali.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyobya, alisema ujio wa vifaa tiba hivyo ni neema kwa halmashauri hiyo.

Alisema, maboresho hayo makubwa yanayofanywa na Rais Dk. Samia ni lazima kuungwa mkono na watendaji na anatoa siku 15 kuhakikisha MSD inafunga vifaa hivyo na wananchi wanaanza kupata huduma.

"Niwaombe MSD ilete wataalamu wao kwa ajili ya kufunga vifaa hivi, haiwezekani Rais wetu afanye mambo makubwa kama haya watendaji tumwangushe, ni muhimu kuhakikisha tunasimamia na wananchi wanaanza kupata huduma kwa wakati," alisema.

Mwakilishi wa MSD ambaye ni Mfamasia na Ofisa Huduma kwa Wateja Kanda ya Dar es Salaam, Diana Kimario, alisema kanda hiyo ina hudumia mikoa mitatu ambayo ni Pwani, Morogoro na Zanzibar ambapo Ifakara ni mnufaika.

"Ujio wa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 900 ni mwendelezo wa mabadiliko makubwa katika maboresho sekta ya afya, sisi watumishi ndani ya MSD tunajivunia namna serikali yetu chini ya Rais Dk. Samia na Mkurugenzi wa bohari Mavere Tukai wanavyohakikisha tunafanya kazi bila hofu.

# EWURA yatangaza neema magari yanayotumia gesi asilia

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), imesema idadi ya vituo vya kujazia gesi asilia kwenye magari itaongezeka hivi karibuni kwa kuongeza kasi ya kutoa vibali na leseni za ujenzi wa vituo hivyo kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, James Andilile, alisema hayo wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu udhibiti wa maji, umeme, gesi na mafuta.

Alisema hivi karibuni EWURA ilifanya utafiti kwenye maeneo yenye vituo vya mafuta kandokando ya bomba kubwa la gesi asilia na kubaini kuwa wamiliki wa vituo hivyo wako tayari kutumia valvu zilizoko kwenye bomba hilo kuingiza kwenye vituo vyao vya mafuta na kuuzia wenye magari.

"Wenye vituo vya mafuta wameonyesha utayari wa kuweka pampu hata moja kwenye kila kituo cha mafuta kwa ajili ya kujaza gesi asilia ambayo watawauzia wenye magari. EWURA inaendelea kutoa vibali leseni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kujaza gesi asilia," alisema Andilile.

Aidha, alisema katika kuhakikisha vituo vya kujazia gesi vinaongezeka kwa kasi, EWURA imekuwa ikishirikiana na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha changamoto yoyote inayojitokeza inapatiwa majibu ya haraka.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amesaidia kukwamua mradi wa gesi asilia (LNG) ambao ukishatekelezwa utasaidia kuimarisha upatikanaji wa gesi asilia kwa matumizi ya majumbani na kuuza nje ili kupata fedha za kigeni.

Alisema kwa taarifa rasmi zilizopo hivi sasa viwanda 54 nchini vinatumia gesi asilia kwa ajili ya shughuli uzalishaji wa viwandani kuendesha mitambo na wananchi 1,515 wa mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Lindi wanatumia gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani.

Alisema serikali inatumia gesi asilia kuzalisha Megawati 1,193 na kwa sasa kuna magari 3,758 ambayo yanatumia gesi asilia kwa kununua gesi kutoka kwenye vituo mbalimbali vinavyouza nishati hiyo.

"Tunamshukuru mheshimiwa Rais Samia kwa kukwamua mradi wa LNG kwasababu utaleta matokeo makubwa kwenye uchumi wetu kwa kiasi kikubwa na utasaidia kuimarisha matumizi ya gesi asilia kuendesha mitambo badala ya kutegemea mafuta ambayo tunaagiza nje ya nchi," alisema.

Alisema kwa sasa kuna vituo vitatu vya kujaza gesi asilia kikiwamo cha Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), na Pan Africa maeneo ya Ubungo, Dangote Mtwara na kituo kingine kilichoko Tazara, jijini Dar es Salaam.

"Kituo cha Dangote kilichoko Mtwara kinahudumia magari karibu 250 ya kiwanda cha Dangote kwa ajili ya kusafirisha saruji mikoani, lakini vituo vya kujazia gesi Dar es Salaam vinahudumia wastani wa magari 350 kwa siku na hivi karibuni kuna kituo kingine kitazinduliwa maeneo ya Airport maana kimekamilika," alisema.

Kuhusu umeme, alisema mradi wa kuzalisha kwa maji kwenye Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere umefikia asilimia 92 na utakapokamilika utazalisha Megawati 2,115.

Alisema mwaka 2015 Tanzania ilikuwa inazalisha Megawati 1,400, lakini kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na serikali sasa inazalisha Megawati 1,900 sawa na ongezeko la Megawati 500.

Alisema miaka ya karibuni Watanzania waliokuwa wameunganishiwa umeme walikuwa asilimia 65, lakini imeongezeka na kufikia asilimia 78 huku idadi ya watumiaji wa nishati hiyo wakiongezeka kutoka watu milioni 2.2 na kufikia milioni 2.4.

"Watu wanaweza kudhani kwamba uwekezaji haufanyiki, lakini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) wamefanyakazi kubwa sana na kwa sasa takribani vijiji 10,000 vimeshaunganishwa na umeme na vijiji vichache vilivyobaki mpaka Juni mwakani vitakuwa vimeunganishwa," alisema.

Aidha, alisema katika jitihada za kupunguza upungufu wa umeme serikali imejielekeza kutafuta vyanzo mbalimbali vya umeme ikiwamo gesi asilia na kwamba asilimia 64 ya umeme unaozalishwa nchini unatokana na gesi asilia.

"Tuligundua gesi asilimia miaka ya 70 Songosongo na mwaka 1982 tuligundua gesi asilia Mnazi Bay na ile ya Songosongo tukaanza kuitumia kwenye uzalishaji viwandani mwaka 2004 wakati ile ya Mnazi Bay tulianza kuitumia mwaka 2006 kwa ujumla matumizi ya gesi asilia yanazidi kuongezeka," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Sababu baadhi taasisi za dini kutosajiliwa zatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema katika kipindi cha miaka saba taasisi na madhehebu ya dini 419 zimesajiliwa kati ya maombi 1,858 yalipokewa na Ofisi ya Msajili wa Jumuiya.

Aidha, imeeleza sababu za baadhi ya madhehebu ya dini kuchelewa kusajiliwa nchini kuwa ni pamoja na kukosa vigezo vya kusajiliwa.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda.

Mbunge huyo alihoji ni maombi mangapi ya usajili wa taasisi na madhehebu ya dini yamewasilishwa tangu 2016 na hazijapatiwa usajili na sababu za kutosajiliwa.

Akijibu swali hilo, Sagini alisema kati ya maombi yalipokewa, taasisi na madhehebu ya dini 419 yamesajiliwa, manne yamekataliwa na 1,435 yapo katika hatua mbalimbali za usajili.

"Sababu zinazopelekea baadhi ya taasisi na madhehebu ya dini kuchukua muda mrefu kusajiliwa au kotosajiliwa ni pamoja na baadhi ya taasisi na madhehebu ya dini kukosa vigezo vya kusajiliwa, kubadili anwani za Posta au Makao Makuu ya taasisi bila kutoa taarifa na hivyo kukosekana kwa mawasiliano.

"Baadhi ya taasisi na madhehebu kukosa maeneo stahiki ya kuendeshea shughuli zao na kuingia kwenye migogoro ya ndani, migogoro na jamii inayozunguka taasisi hizo au mamlaka za serikali zilizopo katika maeneo hayo au kukabiliwa na kesi katika mamlaka za utoaji haki nchini," alisema.

Aidha, wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya inaendelea kushughulikia maombi ya usajili wa taasisi na madhehebu ya dini na kutoa usajili kwa wakati kwa taasisi zenye sifa stahiki.

Pia alisema serikali haisajili taasisi na madhehebu ya dini ambayo yanaweza kuleta madhara kwa jamii au kuhamasisha vitendo ambavyo ni kinyume na mila, desturi, utamaduni na maadili ya kitanzania.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema idadi ya maombi yaliyoshughulikiwa ni ndogo na kuhoji serikali haioni inachukua muda mrefu kutoa uamuzi.

"Je, hamjui zipo athari za kuchelewa kufanya maamuzi haya?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Sagini alikiri kuwa baadhi ya maombi yamechukua muda mrefu kutokana na sababu alizobainisha na pia serikali inataka kujiridhisha kuwa taasisi inayosajiliwa haiwezi kuleta athari nchini.

"Kwa mfano moja ya athari taasisi kushindwa kufungua akaunti benki, kushindwa kumiliki ardhi, wanapoomba kusajiliwa wafuate vigezo wanavyopewa na wataalamu ili isichukue muda mrefu," alisema.



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua kitengo cha walipakodi wa kati, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Kamishna wa Upelelezi wa Kodi, Evarist Mashiba (kushoto), Kamishna wa Kodi za Ndani, Alfred Mregi (wa pili kushoto), Kamishna wa Walipakodi Wakubwa, Michael Muhoja (wa tatu kulia), Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano, Richard Kayombo (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Emmanuel Nnko. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mbunge ahoji utekelezaji mradi maji Makonde

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amehoji mpango wa serikali wa muda mfupi na mrefu wa kukarabati mradi wa maji wa Makonde unaohudumia halmashauri nne za Mkoa wa Mtwara.

Akiuliza swali bungeni jana, Chikota alihoji kazi aliyopewa kwa sasa mkandarasi ni kupeleka maji katika matangi makubwa na hakuna fedha za usambazaji, je, serikali ina mpango gani wa dharura kutenga fedha nyingi za usambazaji kwenye vijiji vya mradi huo.

"Maendeleo ya mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kupeleka Mtwara Manispaa ambao utanufaisha na Halmashauri ya Nanyamba, je, mradi huu utaanza kutekelezwa lini?" Alihoji.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi akijibu, alisema serikali inatambua mradi wa maji wa Makonde ni chakavu na unahitaji ukarabati.

"Katika mpango wa muda mfupi kwa mwaka 2023/24, serikali imetenga Sh. bilioni 1.5 ambapo tayari zaidi ya Sh. milioni 200 zimetolewa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa mabomba na kazi ya ulazaji inaendelea umbali wa kilometa tano umekamilika kati ya 31 zilizopangwa," alisema.

Alisema katika mpango wa muda mrefu, serikali inaendelea na ukarabati mkubwa wa mradi wa Makonde kupitia mradi wa maji wa miji 28 utakaogharimu Sh. bilioni 84.7.

Alisema kuwa utekelezaji wa mradi huo umeanza mwezi Juni, 2022 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2024 na utekelezaji umefikia asilimia 40.

"Kukamilika kwa mradi huu kutaondoa tatizo la maji katika Halmashauri ya Mji wa Newala, Halmashauri ya Wilaya ya Newala, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na Halmashauri ya Mji wa Nanyamba," alisema.

Kadhalika, alisema mpango wa wizara ni kuhakikisha baada ya kukamilika kwa mradi kazi itakayofuata ni usambazaji ambao hufanywa na Mamlaka ya Maji.

Alisema kipaumbele cha wizara ni kuhakikisha mradi wa kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Mtwara unatekelezwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

# Kituo kimataifa biashara Ubungo kuajiri 65,000

**Na Joseph Mwendapole**

UJENZI wa Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki (East Africa Commercial and Logistics Center), ambacho kukamilika kwake kutatengeneza ajira 65,000 unatarajiwa kukamilika na kuanza biashara Juni, mwakani.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Cath Wang, alitoa taarifa hiyo kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji (TIC), Dk. Binilith Mahenge kuhusu maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho ulioanza Aprili, mwaka huu.

Alisema ujenzi utakamilika mwezi Desemba, lakini shughuli ya ukamilishaji wa urembo na mahitaji mengine yatakuwa yamekamilika mpaka Juni mwakani na biashara itaanza kufanyika mara moja.

"Mradi huu ulizinduliwa rasmi mwezi wa nne mwaka huu, lakini mpaka Desemba tutakuwa tumekamilisha jengo lote na tutakuwa tumebakisha urembo tu ambao tutakamilisha mwezi wa sita mwakani na biashara itaanza mara moja," alisema Cath Wang.

Alisema ujenzi wa kituo hicho ni fursa nzuri kwa wafanyabiashara mbalimbali nchini na kusema kuwa wanaotaka kujua zaidi kuhusu uwekezaji huo wanaweza kufika kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali namna ya kupata vizimba.

"Ujenzi huu mpaka mwisho utagharimu Dola za Marekani milioni 110, lakini mpaka sasa tumeshatumia Dola milioni 70 kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ujenzi wa hili jengo ambalo litakuwa na maduka zaidi ya 2,500," alisema Wang.

Aidha, alisema wakati huu wa ujenzi wameshatoa ajira kwa Watanzania 1,500 na kwamba hadi kukamilika jumla ya ajira za moja kwa moja 15,000 na za muda zitakuwa 50,000 na kuwa na jumla ya ajira 65,000.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TIC, Dk. Binilith Mahenge, alipongeza maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho ambacho alisema kitasaidia kuongeza ajira kwa Watanzania na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

Alisema hayo ni matunda ya serikali ya awamu ya sita ambayo imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa kubadilisha sheria na kuendelea kuvutia uwekezaji wa nje na ndani ya nchi kwenye nyanja mbalimbali.

"Serikali imejitahidi kuweka mzingira tulivu ambayo yamekuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji ndiyo sababu mnaona wanaendelea kumiminika kila siku na hakuna mwekezaji anayeweza kuja kuwekeza kwenye mazingira ya vurugu vurugu," alisema Mahenge.

"Hawa wangeweza kupeleka mradi huu Kenya, Uganda, Msumbiji, lakini wameamua kuja Tanzania kwasababu ya mazingira mazuri ya uwekezaji na amani na utulivu uliopo kwa hiyo nasisi TIC tutaendelea kuweka mazingira ya kuwavutia wawekezaji," alisema.

Alisema TIC imekuwa ikifanya kampeni mbalimbali za kuvutia uwekezaji ikiwamo kuwatafutia maeneo ya kujenga viwanda ili wanapokuja nchini wasihangaike kutafute maeneo ya kujenga viwanda vyao.

Alisema serikali imeweka vivutio vingi vya uwekezaji kwaajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na amewakaribisha wawekezaji wa ndani kuchangamkia fursa mbalimbali zinazopatikana hapa nchini.



## IAA kufundisha utambuzi wa magonjwa ya mimea

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA), kimeanza kutekeleza programu maalum kufundisha namna ya kuandaa na kugundua kifaa maalum cha utambuzi wa magonjwa yanayoshambulia mimea, hasa zao la parachichi.

Akizungumza jana, wakati wa kongamano la Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) la mwaka 2023, mwanafunzi Said Hussein, anayesoma Shahada ya Mtandao, alisema wamelazimika kugundua kifaa hicho kutokana na mimea mingi kushambuliwa na magonjwa, na wakulima hawana elimu ya kupambana na magonjwa hayo.

"Tulifikia hatua ya kuanzisha mchakato wa kugundua programu hii baada ya kushuhudia wakulima wa parachichi kule kwetu Mbeya wakiteseka kwa mazao yao kushambuliwa na wadudu na kutokuwa na ujuzi wa kukabiliana na wadudu hao," alisema.

Mkuu wa Chuo cha IAA, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema lengo la kuwakutanisha wadau kutoka ndani na nje ya Mkoa wa Arusha ni ili kujadiliana masuala mbalimbali kuhusu TEHAMA.

Prof. Sedoyeka, alisema kongamano hilo limekuwa chachu katika kuibua vipaji kwa wanafunzi kuonesha kazi zao za ubunifu na uvumbuzi katika TEHAMA na kuwakutanisha na wadau wa sekta hiyo, kujadiliana namna ya kuwawezesha kuweka mazao ya ubunifu wao sokoni.

Alisema katika kuendana na kasi ya serikali ya uwekezaji kwenye TEHAMA, chuo hicho kimejikita na uboreshaji wa miundombinu na kuanzisha mitaala bora ili kutoa wataalamu wenye uwezo watakaokubalika sokoni na watakaotumia elimu na ujuzi kutatua changamoto katika jamii.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA nchini, ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Kiufundi, Jasson Ndanguzi, alisema tume hiyo itaendelea kushirikiana na vyuo vya elimu ya juu kufanya utafiti utakaoibua mwelekeo wa sekta hiyo kutatua matatizo katika jamii na kuibua fursa za kiuchumi pamoja na kuiwezesha serikali kuandaa sera zinazoendana na wakati.

Pia alikipongeza chuo hicho kwa kufanya kongamano hilo na kuahidi kuwa tume hiyo itaendelea kuwasaidia wabunifu wa mifumo hiyo, hususani wanapofikia hatua ya kuipeleka sokoni kwa walaji ili watimize lengo la kuisaidia jamii.

Prof. Edson Lubua kutoka Kitivo cha TEHAMA cha IAA, alisema kongamano hilo limekuwa likitoa motisha kwa wanafunzi na kuonesha thamani ya kazi za bunifu zao pale wanapozionesha kwa walaji ambao ni kampuni, waajiri na taasisi mbalimbali ambazo zinaweza kuwawezesha kufikia ndoto zao.

# Wavuvi waonywa kutobadili matumizi boti walizopewa

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewaonya wavuvi wa Mkoa wa Tanga, waliopewa boti za kisasa 14 zenye thamani ya Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya shughuli za uvuvi katika ukanda wa kiuchumi wa bahari, kutojaribu kubadili matumizi yake.

Alisema serikali itakuwa macho wakati wote kutizama matumizi yake, kwa kuwa wako wanaoweza kuzigeuza kuwa boti za biashara ya kupeleka watu kuogelea katikati ya Bahari ya Hindi.

Ulega, alikwenda jana jijini Tanga kukabidhi boti hizo kwa wanachama 225 wanaounda vikundi vya uvuvi kutoka wilaya za Pangani, Mkinga, Muheza na Tanga. Boti hizo ni mkopo wa masharti nafuu, uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB).

"Nendeni mkazifanyie kazi na mpate mafanikio na kurudisha mkopo na siyo kwa matumizi mengine. Kule baharini, kuna wale wanaofanya uvuvi haramu, tunataka mkapambane nao, isiwe mna vyombo vya kisasa, halafu samaki wanaharibiwa kwa mabomu.

...Muwe namba moja kupambana nao, maana tunataka mkavue samaki na siyo kwenda kuogelea, isitoshe na ninyi mna boti za kisasa zenye uwezo wa kukimbia kwa kasi."

Katika mgawo huo, boti sita zimekabidhiwa kwa wavuvi wa Wilaya ya Pangani, Wilaya ya Mkinga boti nne, Wilaya ya Muheza boti tatu na Tanga boti moja.

Kwa mujibu wa Waziri Ulega, Rais Samia Suluhu Hassan, amepanga mpango huo kuwa endelevu, tayari ametenga Sh. bilioni 25 kwa ajili ya wavuvi.

Awali, Msemaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Dk. Kanael Nnko, alisema benki hiyo imeweka mpango mkakati wa kuchangia mapinduzi ya sekta ya mifugo na uvuvi nchini.

"Kupitia mradi huu, TADB imeshapokea Shilingi bilioni 25.175 kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba, kwa wanufaika wa boti za kisasa, kilimo cha mwani na wafugaji wa samaki," alifafanua Dk. Nnko.



Baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Elijerry (ECOHAS), wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakipita kwa tabu kwenye daraja la magogo la Mto Msangazi, jirani na chuo hicho jana, lililoharibiwa na mafuriko ya mvua zinazoendelea kunyesha, ambapo wameiomba serikali kujenga daraja la kudumu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wakurugenzi saba wawekwa 'mtegoni' ripoti ya CAG

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, amesema hoja za ukaguzi zinazotokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ambazo hazina majibu ni 'mtego' kwa wakurugenzi saba wa halmashauri zake.

Akizungumza jana katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa huo (RCC), Babu, alisema halmashauri yoyote itakayoshindwa kujibu hoja za CAG, mkurugenzi wake yuko matatani.

"Hakikisheni mnajibu hoja zote za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali zilizopo, lakini pia msizalishe hoja ili halmashauri zetu zipate hati safi.

"Aidha, atakayeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato, ajiandae kuwajibika. Yale yote yaliyopangwa kufanyika kwa mwaka wa fedha 2023/2024, yakamilishwe kwa asilimia 100.

...Kwa taarifa nilizonazo hadi sasa, halmashauri zimekusanya Sh. bilioni 9.502 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato, sawa na asilimia 33 ya lengo la makusanyo kwa mwaka 2023/24, ambalo ni shilingi bilioni 28.95."

Alisisitiza kuwa taarifa ya mapato aliyonayo hadi mwezi Oktoba, mwaka huu, inaainisha ufanisi wa kila halmashauri katika ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa kulinganisha makisio idhinishwa na mapato halisi.

Kwa mujibu wa TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), wakurugenzi wa halmashauri zilizokusanya mapato chini ya asilimia 75 wanatakiwa kujitathmini, endapo wanatosha kuendelea kuziongoza halmashauri hizo.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alisema kutokana na hatua alizoanza kuchukua Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu ripoti ya CAG, anatuma ujumbe kwamba kwenye mambo ya msingi, yenye manufaa kwa nchi, hakuna jambo la urafiki au ukaribu na mtu.





# Diwani Msalala alalamika vibarua REA kutokulipwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

DIWANI wa Kata ya Mega, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, Patrick Mazuri, ameiomba serikali kupitia Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA), kuwalipa vibarua walioshiriki katika uchimbaji wa mashimo wakati wa usimikaji nguzo katika Kata ya Mega.

Aliwasilisha malalamiko ya vibarua hao juzi wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/2024, na kusema kuwa baada ya kazi hiyo vijana hao hawakulipwa.

Alisema vijana hao walipewa vibarua kwa makubaliano ya kulipwa Sh. 520,000 lakini licha ya kukamilisha kazi hawajalipwa hali inayowakatisha tamaa ya kuendelea kushiriki katika mradi huo katika maeneo mengine.

Diwani Mazuri alisema, Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) linatakiwa kabla ya mkandarasi kuondoka katika eneo la mradi, awe amelipa malipo ya vibarua alioshirikiana nao utekelezaji wa mradi ili kusaidia kuondoa malalamiko.

Hata hivyo, kikao hicho hakikuwa na mwakilishi yeyote kutoka Tanesco wala REA hali iliyomsikitisha Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita na kutoa onyo kwa taasisi zote kuweka wawakilishi katika vikao vyote vya mabaraza ya madiwani kwa ajili ya kujibu kero za wananchi.

Aidha, aliahidi kufuatilia malipo hayo kwa Meneja wa Tanesco ili kujua kwanini mkandarasi hakuwalipa vijana walifanyakazi ya kuchimba mashimo ya kusimika kwa nguzo na mradi umeshakamilika.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Hamisi Katimba, alieleza kupokea malalamiko hayo kabla na kwamba amelifuatilia ili kuhakikisha malipo yanapatikana kwa wakati na muda wowote vibarua hao watalipwa na kuondoa sintofahamu.

Mbunge wa Msalala Iddi Kassimu aliwataka wakandarasi wanaofanyakazi katika halmashauri hiyo, kuwalipa wafanyakazi wao mapema ili waendelee kufanyakazi katika miradi iliyopo kwenye kata zao badala ya kulimbikiza madeni.

Alisema, Waziri wa Nishati Dk. Dotto Biteko, aliahidi kuweka mikakati mikubwa ya kuhakikisha kuwa umeme unawaka kata zote 18 na vijana wataendeela kupewa kipaumbele kwa kazi za muda zisizohiotaji ujuzi ili kujiingizia kipato.




Mkurugenzi wa Fedha wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Dk. Kaanael Nnko (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza taarifa za fedha za benki hiyo kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka ambapo imepata faida ya Sh. bilioni 4.88 kabla ya kodi. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo na Biashara wa benki hiyo, Afia Sigge na Meneja wa Mifuko ya Wakala, George Nyamrunda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC aitaka halmashauri kuchangamkia fursa chuo kikuu

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Tabora, Lous Bura, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Elias Kayandabila, kuchangamkia fursa ya Mradi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu Cha Mwalimu Nyerere katika maeneo ya Kata ya Itonjanda, Wilaya ya Uyui kwa kuweka miradi ya vitega uchumi kabla ya nafasi kuchukuliwa na wawekezaji wengine.

Alisema hayo juzi wakati wa kikao na wadau wa elimu wilayani hapa kuwa kama halmashauri isipochangamkia fursa hiyo wawekezaji wengi kutoka sehemu mbalimbali watakuja kuvizia ili wawekeze katika maeneo hayo ya chuo na kukosa vyanzo vya mapato.

Alisema halmashauri ina uwezo mkubwa wa kujenga majengo mbalimbali kwa ajili ya kujiingizia mapato kwa kuwa sera yao ni kutoa huduma kwa jamii na kuingiza kipato kwa halmashauri.

Mratibu Elimu wa mageuzi ya kiuchumi, Profesa Msafiri Jackson, akizungumza katika kikao hicho alisema mradi huo utatekelezwa na serikali katika eneo lenye ekari 150 na utagharimu Dola za Kimarekani milioni 425.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Elias Kayandabila, alisema amepokea maelekezo hayo na kuahidi kuyatekeleza ikiwa ni pamoja na kuandaa miundombinu itakayowezesha shughuli za chuo hicho kufanyika kwa ufanisi.

**Alisema halmashauri ina uwezo mkubwa wa kujenga majengo mbalimbali kwa ajili ya kujiingizia mapato kwa kuwa sera yao ni kutoa huduma kwa jamii na kuingiza kipato kwa halmashauri.**

# Viongozi wanaotuhumiwa kuhujumu Sh. milioni 29 wasimamishwa kazi

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

VIONGOZI wawili wa Chama cha Ushirika cha Wachimbaji Madini (IPONYABUHABI) akiwamo Makamu Mwenyekiti Simon Mwita, wamesimamishwa uongozi katika chama hicho ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za kuhusika na wizi wa gramu 200 za dhahabu zenye thamani ya Sh. milioni 29.

Vilevile, ushirika huo umemsimamisha pia mjumbe wa bodi, Elizabeth Glalani, pamoja na mmoja wa wanachama wa chama hicho ambaye hakutajwa kwa jina wakikabiliwa na tuhuma za ubadhirifu pamoja na katiba ya chama hicho.

Akithibitisha hatua hiyo juzi Mwenyekiti wa Ushirika huo, Emanuel Gambi, alisema mkutano mkuu maalum wa ushirika huo ulioitishwa kwa maelekezo ya Ofisi ya Mrajisi Msaidizi wa vyama vya ushirika Mkoa wa Geita, ulifikia hatua hiyo baada ya kuwapa fursa ya kutoa utetezi wao kabla ya kusimamishwa.

Gambi alisema, dhahabu hiyo ilinusurika kuhujumiwa baada viongozi hao kudaiwa kujaribu kula njama kufisadi na kuuzwa kinyemela bila ya kufuata taratibu za katiba na ushirika huo ambampo hata hivyo ilikamatwa na msimamizi wa shimo namba 10, Masuke Mudo.

Alidai kuwa tukio la wizi wa dhahabu hiyo uliratibiwa na viongozi hao kwa kumtuma mmoja wa wanachama wa ushirika ambaye hata hivyo alikamatwa na kunyang'anywa dhahabu hiyo.

Meneja Mkuu wa chama hicho cha ushirika George Kasaiza, alisema hatua ya kusimamisha viongozi hao inalenga kupisha uchunguzi ikiwa ni pamoja na tuhuma zingine zikiwamo za kukiuka katiba na sheria za ushirika huo pamoja na njama za wizi wa dhahabu hiyo.

Baadhi ya wachimbaji wadogo katika mgodi huo wakiwamo Aldi Erasto na Tabu Hassan, walisema kuwa kero zinazojitokeza katika mgodi huo zinatokana na baadhi ya viongozi wa ushirika huo kukosa uadilifu.

Alipotafutwa Makamu Mwenyekiti aliyesimamishwa kwa tuhuma hizo, Mwita na Elizabeth kuzungumzia tuhuma hizo kwa nyakati tofauti walikana kuwapo kwa wizi wa dhahabu wala kuhusika na kueleza kuwapo kwa mgogoro uliosababisha kusimamishwa kwao na kuahidi kutoa utetezi wake wakati wa taratibu za uchunguzi.

Mwita alikiri kusimamia uzalishaji wa dhahabu inayolalamikiwa na kuwa baada ya kuzalishwa kutoka shimo namba 10 chini ya usimamizi wake aliiuza fedha iliyopatikana aligawanya ikiwamo Shilingi milioni nane kwa ajili ya ushirika na kiasi kingine kuwapatia wachimbaji.



Ukurasa 12

**RC Mara alivyomaliza danadana ya h/shauri kuzikwepa ofisi mpya**



Ukurasa 13


Bandari ya Dar ilivyo lango la kufikia mtangamano Afrika

siasa

JUMATANO NOVEMBA 8, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU



Ukurasa 14

UCHAGUZI MAREKANI

**Ni hatihati kwa Rais Joe Biden, chatabiriwa kishindo kwa Trump**

MIAKA MITATU MADARAKANI SMZ

# Ndivyo Rais Mwinyi anavyotunzwa tuzo Ulinzi wa Kinamama, Watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MIONGONI mwa mafanikio ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi tangu kuingia madarakani Novemba 2021, ni kujali na kutetea haki za wanawake na watoto wanaodhalilishwa.

Anaona umuhimu huo na kuanzisha mahakama maalum ya kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia, ambazo zinaligusa zaidi kundi hilo.

Kuundwa kwa mahakama hiyo ni ili mashtaka hayo yasikilizwe kwa haraka na haki kuonekana ikipatikana na kukomesha matendo hayo yanayochafua utu wa mtu.

Kabla ya uongozi wake kesi za namna hiyo zilikuwa zikisikilizwa katika mahakama za kawaida na hakukuwa na mahakimu maalum hali iliyopelekea kuwepo kwa mrundikano mkubwa wa mashauri na kuchukua muda mrefu kutoa hukumu.

Katika miaka mitatu ya kuanzishwa kwake, Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, kinafanya utafiti unaolenga ufanisi wa mahakama hiyo maalum katika kushughulikia kesi za udhalilishaji tangu ilipoanzishwa.

Utafiti huo pia unalenga kupata maoni ya nini kifanyike kuimarisha mifumo ya utoaji haki kwa lengo la kusaidia kupunguza au kutokomeza unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto Zanzibar.

Anapowasilisha ripoti ya utafiti huo, Hawra Shamte kutoka TAMWA, anasema wahojiwa kutoka shehia 60 za Unguja na Pemba, wanatoa maoni tofauti kuhusu utendaji wake, wengine wakiisifu na baadhi wakisema hawajaridhishwa.

"Hata hivyo watu ambao walisema hawakuridhishwa na hukuma inayotolewa na mahakama maalum ni wale ambao hukumu zilizopotoka hazikuwatia hatiani washitakiwa,"anasema Hawra.

Aidha, waliosema wameridhika na mahakama hiyo ni kutokana na uharaka wa kuendesha kesi, kupunguza usumbufu wa wahasiriwa kwenda na kurudi kwa muda mrefu na hukumu zinazotolewa wanaona ni za haki.

Anasema utafiti huo pia unaonyesha kuwa tangu 2021 hukumu zinazotolewa ziliongezeka, lakini baadhi ya mahakimu bado wanahukumu kifungo cha miaka miwili jela kinyume na maelekezo ya sheria.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, mwaka 2021 kulikuwa na matukio 1,222 ya udhalilishaji ambayo yalifikishwa mahakamani na kesi 261 washitakiwa wamefungwa na kesi 51 wameachiwa.

Mwaka 2022, matukio 1,360 yaliripotiwa, kati ya hayo 534 yapo chini ya upelelezi wa polisi, mengine mawili yanashughulikiwa na Ofisi ya Mwendesha Mashataka (DPP), 421 yapo mahakamani wakati 181 yalihukumiwa.

Kesi nyingine 139 washtakiwa waliachiwa huru, nyingine 19 hazikuwa na mtuhumiwa na nyingine 64 hakuna hatua iliyochukuliwa.

Mratibu wa miradi ya kupinga udhalilishaji TAMWA, Zaina Salum, anasema katika kuendelea na kampeni ya kupaza sauti ya haki za watoto dhidi ya matukio ya ukatili, chama kinafanya tafiti mbalimbali ili kukuza uchechemuzi wenye kuchochea mabadiliko chanya.

Zaina anasema watoto wote wanastahili kulindwa dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na kupata haki zao katika vyombo vya sheria.

Sabaha Bakari mwanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji mkoa wa Kusini Unguja, anasema katika mahakama maalum ya udhalilishaji kesi zinachukuliwa kwa uzito na hata hukumu zinazotolewa si ndogo kama ilivyokuwa awali.

"Siku hizi utasikia mtu anapewa kutoka kifungo cha miaka 20 hadi 60 na pia wapo waliofungwa maisha,"anasema.

Aidha, anasema bado kuna changamoto katika utoaji wa hukumu hizo, mfano katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita kulikuwa na kesi 20 katika mahakama ya mkoa Mwera lakini 16 watuhumiwa wameachiwa huru na kesi mbili ndizo ziliwapata na hatia.

Fatma Khamis Ali, mwanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, anasema baadhi ya kesi huchukua muda mrefu kukamilika.

"Ukosefu wa ushahidi ni changamoto ambayo inazikumbana kesi nyingi za udhalilishaji, washtakiwa wengi wameachiliwa haswa katika kesi ambazo zimedumu kwa muda mrefu,"anasema Fatma ambaye pia ni msaidizi wa sheria.

Aidha, anasema changamoto nyingine ni kwamba waendesha mashtaka wanaona ugumu wa kukata rufaa, hivyo waathiriwa hubakia kutoridhishwa na maamuzi ya mahakama na kukosa matumaini ya kupata haki.

Hija Masoud Ame, mwanamtandao wa kupinga udhalilishaji Wilaya ya Kusini Unguja, anasema ucheleweshaji bado upo tofauti na lengo la kuanzishwa mahkama maalum, pia kesi huahirishwa mara kwa mara.

Hija anasema polisi wanapohamishwa au wakiwa likizo kesi hucheleweshwa kwa sababu jalada likisimamiwa na askari mmoja ndiye anatakiwa kulishughulikia mpaka kesi ikamilike hivyo akipangiwa kazi nyingine mashtaka yatakwama.

Pia anasema miundombinu katika mahakama hiyo haitoshi, kutokana na kukosekana kwa vyombo vya kisasa vya usikilizaji wa kesi, kwa mfano video conference, ukosefu wa vyumba maalum vya kuweka watoto waliohasirika na vitendo vya udhalilishaji ili mtoto asionekane na mshtakiwa.

Aidha anasema majengo ya mahakama hayaridhishi, yamezeeka na hayako katika hali bora na pia hakuna samani za kutoshaakitaja viti.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kufungua Mahakama Kuu iliyoko Tunguu, Unguja. **PICHA: IKULU**

INAENDELEA UK. 13

# RC Mara alivyomaliza danadana ya halmashauri kuzikwepa ofisi mpya

• Awaambia kazi bado, sasa kutinga wilayani Bunda




Mkuu wa Mkoa wa Mara (wa pili kushoto), akisimamia uhamaji wa watumishi wa halmashauri hiyo kutoka Kijiji cha Mugango. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

KUTOA visingizio kuwa kazi hii itafanyika baadaye au kesho ni mazoea ya baadhi ya Watanzania ambao huahirisha mambo bila kujali muda wala gharama kwao ni suala la kawaida.

Lakini, ahadi hewa na wakati mwingine kudanganywa na watendaji wa aina kama hiyo ni kisa ambacho Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, safari hii anakikataa.

Hivi karibuni katika kufuatilia utendaji kazi wa halmashauri zake, saa 2:00 asubuhi, anatinga ghafla katika ofisi za muda za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

Zikiwa katika Kijiji cha Mugango, anazitembelea asubuhi na mapema baada ya watu kuingia kazini, kutaka kushuhudia kama watumishi wa halmashauri hiyo wametimiza ahadi ya kuhamia kwenye makao mapya ya wilaya hiyo yaliyoko Kijiji cha Suguti.

Mtanda anafuatilia watumishi hao wanaoongozwa na Mkurugenzi Msongela Palela, iwapo kama walivyoahidi kuhamia makao mapya wametimiza wajibu.

Hata hivyo, anakuta hakuna dalili za kuhama, na kuamua kuweka 'kambi' eneo hilo, ili kuwasimamia wahamishe vifaa vya kazi kisha wote waondoke kwenda katika ofisi mpya za halmashauri hiyo.

Akizungumza na gazeti hili wakati akiendelea kusimamia zoezi hilo, anasema alimwagiza Mkurugenzi Palela na kumwambia kuwa hataondoka hadi ahakikishe watumishi wote wa halmashauri hiyo wamehamia ofisi za makao makuu mapya kuendelea na kazi vinginevyo, asingekuwa tayari kupokea maelezo tofauti.

Mkuu wa Mkoa anasema baada ya kuona wameondoa vifaa vyote, naye alikwenda makao makuu mapya ya ofisi za halmashauri hiyo na kuweka 'kambi', huku akisema atakuwapo hadi kieleweke ili watumishi wamalize kupanga vifaa ofisini na siku zinazofuata waanze kuhudumia wananchi.

> Jafo hakuishia hapo, alizigusa pia Halmashauri ya Wilaya Arusha, Wilaya Kondoa, Halmashauri ya Wilaya Geita, Iringa na Halmashauri ya Wilaya Mufindi.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (kushoto), akizungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, Msongela Palela, baada ya kufika makao makuu mapya ya halmashauri hiyo yaliyoko Kijiji cha Suguti.

Anaeleza kuwa alichukua uamuzi huo kutokana na ahadi ya viongozi wa halmashauri hiyo kwamba Oktoba 10, wangehama, lakini alipowatembelea katika ziara ya ghafla akakuta bado wapo, kukiwa hakuna dalili za kutekeleza ahadi yao.

"Kwa hiyo nimewaambia kuwa siondoki hadi kieleweke, najua kulikuwa na ucheleweshaji wa hapa na pale, baadhi ya watumishi hawataki kuhama, sijui kwa sababu wamezoea Mugango, lakini wanasiasa pia walikuwa na mkakati wa kukwamisha zoezi la kuhamisha serikali kutoka eneo hilo," anasema Mtanda bila kufafanua.

Mkuu wa Mkoa anawakumbusha watumishi na wanasiasa wenye mitizamo kinyume au tofauti kuwa ndani ya utumishi wa umma kuna maelekezo ya serikali, na kwamba hayatakiwi kujadiliwa, bali kinachotakiwa ni utekelezaji tu.

"Nimewapa maelekezo kuwa sitoki hadi kieleweke, wapange vifaa vya kazi katika ofisi zao mpya halafu kesho waanze kazi kutoa huduma kwa wananchi," anasema.

Aidha, anawapongeza Halmshauri ya Tarime kuwa hakutumia nguvu, bali kutoa maagizo ya kuhamia jengo jipya wakatekeleza mara moja, na kwamba wanaosuasua hawezi kuwafumbia macho.

Baada ya kumaliza kazi ya kusimamia kuhama kwa watumishi hao, anasema kituo kinachofuata sasa ni Halmashauri ya Bunda DC, kwa maelezo kwamba watumishi wa huko hawajahama wakati jengo la ofisi zao limekamilika.

**OFISI ZINAVYOHAMISHWA**

Oktoba mwaka 2019 serikali iliagiza halmashauri 31 ambazo majengo yao yapo nje ya maeneo yao ya utawala kuhamisha ofisi kwenda kwenye sehemu za utawala ndani ya siku 30 kuanzia Oktoba 7, mwaka huo.

Agizo hilo likitolewa na aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI wakati huo, Selemani Jafo, akiongea na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya Sumbawanga mkoani Rukwa.

Anazitaja halmashauri hizo kuwa ni pamoja na ile ya Wilaya Mbeya, Kilombero, Mtwara, Masasi na Halmashauri ya Wilaya Newala.

Mbali na hizo, nyingine ni Wilaya ya Njombe, Kibaha, Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya Mbinga na na ile ya Wilaya Shinyanga.

Kwenye msururu huo, alitaja pia Halmashauri ya Wilaya Bariadi, Wilaya Singida, Nzega, Korogwe na Handeni.

Jafo hakuishia hapo, alizigusa pia Halmashauri ya Wilaya Arusha, Wilaya Kondoa, Halmashauri ya Wilaya Geita, Iringa na Halmashauri ya Wilaya Mufindi.

Zipo Wilaya Bukoba, Mpanda, Kasulu, Kigoma, Moshi na Lindi. Vilevile, zilikuwamo Wilaya Babati, Mbulu, Musoma, Bunda na Tarime.

Waziri Jafo ambaye sasa amehamishiwa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira ), anataja sababu za kuhamisha halmashauri hizo kuwa ni wakurugenzi kutembea kilomita takribani 95 kwenda na kurudi ili kuwahudumia wananchi.

Kutokana na mazingira hayo ya umbali wa vituo vya kazi ambayo pia ni gharama, kwa serikali akasema wakiwa karibu na wananchi adha zinawakera wakazi wa wilaya hizo zikiwamo za kuchelewa kupata huduma zinaweza kushughulikiwa na hata kupatiwa ufumbuzi.

Baada ya agizo Halmashauri ya Musoma ilihamia kwa muda katika Kijiji cha Mugango kusubiri ujenzi wa ofisi za makao makuu katika Kijiji cha Suguti ambazo kwa mujibu wa Mkuu wa mkoa Said Mtanda zimekamilika.

Tangu wakati huo, Mtanda anasema watumishi ambao wamehama bila usumbufu ni wa Halmashauri ya Tarime, na kwamba kwa kuwa amemaliza kusimamia uhamaji wa Halmashauri ya Musoma, sasa nguvu inaelekezwa Bunda ili nao wahamie ofisi ambazo nazo zimekamilika.

# Bandari ya Dar ilivyo lango la kufikia mtangamano Afrika

**Na Gaudensia Mngumi**

MTANGAMANO au ushirikiano kimaendeleo wa kikanda wa Afrika Mashariki na Kusini, unazidi kuimarika baada ya kukamilika kwa mradi wa kimkakati wa ujenzi wa bandari kavu ya Kwala, ambayo ni tawi la Bandari ya Dar es Salaam.

Serikali inatangaza kuwa Kwala iko tayari kutumiwa ili kuhudumia shehena za Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Malawi, Uganda na wageni kama Sudan Kusini na Zimbabwe, anasema Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Professa Godius Kyaharara, anapozuru bandari hiyo mwishoni wiki.

Anafahamisha kuwa bandari hiyo ni lango la kibiashara linashughulikia shehena takriban zote za biashara za kimataifa za hapa nchini lakini pia inahusika na kuyategemeza kiuchumu mataifa yasiyo ya bahari ya nchi wanachama wa Ushoroba wa Kati (central corridor) ya Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Malawi na Uganda kupitia sekta ya uchukuzi na usafirishaji.

Nchi hizo hutegemea bandari ya Dar kuwafikishia bidhaa muhimu kama mafuta, vipuri,malighafi viwandani, mbolea, dawa za watu na mifugo,vifaa vya ujenzi na vya kielekitroniki, mavazi na magari, hivyo lango hilo ni moyo wa uchumi wa mataifa hayo.

Hii inamaanisha kuwa ukamilfu wa bandari ya Kwala ni kuimarisha mtangamano wa Afrika Mashariki EAC na Kusini SADC na kuuweka utayari wa Afrika kwenye masuala ya kutekeleza mkataba wa Eneo la Soko Huru la Biashara la Bara Afrika (AfCFTA).

Bandari ya Kwala iko mkoani Pwani umbali wa kilometa 90 kutoka Bandari ya Dar es Salaam, na ni moja ya mafanikio ya kisiasa na kiuchumi kwenye mtangamano wa Afrika kwa kufanikisha ongezeko la biashara kati ya nchi za Mashariki, Kati na Kusini na kuinua uchumi wa kanda hizo.

"Bandari hii kavu inaziunganisha nchi jirani na lengo ni kuhudumia shehena ya makontena yanayokwenda kwenye mataifa hayo. Lakini haiishii hapo pia tumeshatenga maeneo maalum kwa ajili ya wateja wetu hao wanaotumia Bandari ya Dar.Ni Burundi, Rwanda, Uganda, Malawi, Sudan Kusini na Zimbabwe wote tunawapata hekari 10 kwa ajili kushughulikia shehena zao. Lakini kwa Zambia na DRC kila nchi imetengewa hekta 20,"anasema Katibu Mkuu Kahyarara.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Prof. Godius Kahyarara. **PICHA: MTANDAO**

Anaongeza kuwa biashara katika bandari hiyo na huduma zake ni sawa na zile zinazotolewa katika bandari ya Dar es Salaam na kwamba wateja wanahudumiwa kidijitali na lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa bandari zinafanyakazi kwa ufanisi kuwezesha bidhaa na huduma kuyafikia masoko ya mbalimbali hasa kwenye mataifa wananchama wa Ushoroka wa Kati.

Katibu Mkuu anasema Zambia na Malawi, zimeomba kujiunga na ushoroba huo na kikao cha mawaziri moja ya ajenda ni kuwapa uanachama, kwani wameona kuna faida na maslahi ya kuwa nao, kwa vile lengo la ushoroba wa kati ni kusaidia bandari ya Dar es Salaam kupata shehena ya kutosha na vile vile kuhudumia nchi majirani zinazoizunguka.

Anaeleza kuwa mawaziri hao watakutana mwishoni mwa mwezi huu.

Anasema serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, inakazania uwekezaji na biashara ambao unashika sekta zote ikiwamo ya usafirishaji. Ambayo ni kubwa inayoliingiza taifa fedha nyingi za kigeni ikichuana na utalii na madini lakini utalii sehemu kubwa ni usafirishaji.

Wakati serikali ikitangaza utayari wa Kwala, Bandari ya Dar inatajwa kuboresha viwango vyake vya utoaji huduma, kwa mujibu wa Benki ya Dunia, (WB) ikutumia Kiashiria cha Utendaji Kazi wa Bandari kwenye Makontena (CPPI).

Wakati 2022 ilishika nafasi ya 361 kati ya bandari 386. Mwaka huu ipo nafasi ya 312 kati ya bandari 348, taarifa iliyotolewa Mei 2023 na WB inaongeza.

> Wakati 2022 ilishika nafasi ya 361 kati ya bandari 386. Mwaka huu ipo nafasi ya 312 kati ya bandari 348, taarifa iliyotolewa Mei 2023 na WB inaongeza.

### KUMALIZA FOLENI

Mojawapo ya mambo yanayokera wateja wa Bandari ya Dar ni foleni barabarani, kwa vile shehena ni lazima zitoke bandarini zipite kwenye barabara za Kilwa, Mandela na Morogoro ambazo mara nyingi malori hayo yamekuwa chanzo cha foleni.

Kwa hiyo ujenzi wa bandari ya Kwala utamaliza shida ya foleni si bandarini pekee bali hata barabarani kwa kuwa kiasi kikubwa cha malori kinachoingia na kutoka mjini kitapunguzwa kwa vile yatapakua na kupakia shehena Kwala iliyoko karibu kilometa 90 kutoka katikati ya jiji.

Tanzania nchi ya pili kwa uchumi mkubwa zaidi Afrika Mashariki, itatumia fursa ya kuwa na bandari kuunganisha bomba kutoka Uganda na kusafirisha mafuta ghafi ng'ambo kupitia bandari ya Tanga.

### MKAKATI SGR

Uwepo wa mradi mwingine wa kimkakati wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR sasa unazidi kuiweka Tanzania kwenye ramani ya mataifa yanayofanikisha kukuza uchumi, maendeleo ya kibiashara na kufanikisha mikataba mbalimbali ya kikanda ya siasa za mtangamano Afrika.

Kaimu Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Focus Sahani, anasema shirika litahudumia shehena kutoka melini hadi bandari kavu ya Kwala kwa gharama nafuu na kwamba tayari njia za reli ya zamani 'meter-gauge railways' (MGR) na SGR zimeshaweka matawi ndani ya bandari hiyo.

Makoye anasema katika awamu hiyo ya kwanza zimejengwa laini au njia tano ambazo kila moja ina uwezo wa kubeba mabehewa 20 na kwa maana hiyo njia zote kwa wakati mmoja zinaweza kubeba mabehewa 100 ndani ya bandari hiyo kwa kutumia reli ya MGR.

Wanategemea kwenye awamu ya pili ya ujenzi kujenge njia za kuwezesha treni kuingia na kutoka lakini kuweka matawi ya reli ya SGR ili treni zote mbili ziingie na kuhudumia shehena, anasema Sahani.

Katika moja ya changamoto zilizokuwa zinalalamikiwa kwenye kuhudumia shehena kwenye bandari hiyo ni gharama kubwa zinazotozwa lakini Sahani anasema hilo limemalizika.

Katika ziara hiyo ya Katibu Mkuu wa Uchukuzi, Sahani anasema TRC imeshusha gharama za usafirishaji na kwamba behewa moja lenye kontena mbili litasafirishwa kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi Kwala kwa dola 250, akiongeza kuwa makotena yanayosafirishwa yana urefu wa futi 20.

Kwa kuwa Tanzania imeamua kuwa geti au lango la kufanikisha maendeleo ya kiuchumi na kibiashara kwenye ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini ni wakati wa kuhakikisha kuwa wapo wafanyikazi wenye ujuzi wa kuhudumia wateja kwa uhakika na weledi.

Aidha, serikali kama inavyopanua miundombuni bandari kuanzia kina na sehemu ya kupokelea na kutunza shehena ni lazima pia kuweka teknolojia ya sasa ya kushughulikia idadi inayoongezeka ya shehema kwa ili kufikia lengo la kuihudumia Afrika mashariki na kusini kibiashara kwenye sekta ya usafirishaji na uchukuzi.

## Ndivyo Rais Mwinyi anavyotunzwa tuzo ulinzi wa kinamama, watoto

**INATOKA UK. 11**

### HISTORIA

Januari 2021 Rais Mwinyi alitangaza kwa umma umuhimu wa kuanzishwa mahakama maalum kama hatua ya kukabiliana na vitendo hivyo vya udhalilishaji.

Kipindi hicho Dk Mwinyi akasisitiza: "Iwapo kuna watu ambao watahukumiwa kifungo cha maisha au miaka 30 jela, itakuwa mfano kwa wengine, tuonyeshe kuwa hili ni jambo ambalo tunalichukia..."

Kwa kuzingatia hilo, June, 2021, mahakama maalum ilianzishwa rasmi, ambayo inashughulikia kesi za uidhalilishaji pekee na kwa sasa kuna mahakama tano chini ya mahakimu wanane wanaoshughulikia kesi za udhalilishaji, tatu zipo Unguja na mbili Pemba.

Mahakama hiyo maalum ambazo ilianza kufanya kazi mwaka 2011 na kuwekwa kwa mahakimu maalum ambao kazi yao ni kusikiliza kesi za udhalilishaji pekee na sio nyingine kama ilivyokuwa awali kabla ya kuanzishwa.

Wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto wanasema kuazishwa kwake, hivi sasa kusikiliza kesi kunakwenda kwa kasi na hukumu zinazotolewa zinaridhisha tofauti na hali ilivyokuwa kabla.

### CHANGAMOTO

Kukosekana ushahidi kunatajwa kuwa ni changamoto kubwa na kesi nyingi, Khamisi Silima Hakimu wa Mahakama katika mahakama hiyo Mkoa wa Mjini Vuga, anasema.

Anaongeza kuwa kuanzishwa mahakama maalum ya udhalilishaji Zanzibar, kumefanikisha kesi za udhalilishaji kuingizwa kisheria kwenye kundi la makosa ambayo hayana dhamana.

UCHAGUZI MKUU MAREKANI

# Ni hatihati kwa Rais Joe Biden, chatabiriwa kishindo kwa Trump

• Yanayoelekea kumng'oa ikulu uzee, Israel, kuvuruga uchumi



Rais wa Marekani, Joe Biden (88) na mpinzani wake Donald Trump (77), wote ni wazee lakini kuna anayepewa nafasi zaidi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

NI mwaka mmoja sasa umebakia kufikia uchaguzi mkuu wa Marekani, dunia ikianza kuelekeza macho na masikio kwa taifa hilo kubwa unaofanyika Novemba 2024 kuchagua rais na magavana wa majimbo 52.

Hata hivyo Rais Joseph au Joe Biden anaonekana kupitwa na mgombea wa Republican Donald Trump katika majimbo matano muhimu kati ya sita kwenye uwanja wa uchaguzi wa Marekani hasa kwenye kura za maoni majimboni.

Hata hivyo, Wamarekani wengi wanaeleza mashaka yao kuhusu umri wa Biden na kutoridhishwa naye jinsi anavyoshughulikia uchumi, kura za maoni za hivi karibuni zinasema, kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters.

Trump, mtia nia ambaye chama chake kinatarajia kumteua kwenye uchaguzi wa 2024 ili arejee Ikulu ya White House, anaongoza katika majimbo ya Arizona, Georgia, Michigan, Nevada na Pennsylvania, huku Biden akiwa mbele katika jimbo la Wisconsin, matokeo ya kura za maoni Jumapili iliyopita yalionyesha.

Rais Biden alimshinda Trump katika majimbo yote sita mnamo 2020, lakini Trump sasa anaongoza kwa wastani wa asilimia 48 hadi 44 katika majimbo hayo, kura za maoni zinaonyesha, Reuters inasema.,

> Niwaombe linapotokea suala la kitaifa tuwe kitu kimoja badala ya kuungana na adui zetu kuumizana wenyewe kwa wenyewe.

Ushindi wa Biden katika majimbo ya Arizona, Georgia, Michigan, Pennsylvania na Wisconsin - majimbo yote ambayo Trump aliyabeba uchaguzi wa 2016 ulikuwa muhimu katika ushindi wake wa 2020. Biden huenda angehitaji kuyabeba majimbo mengi zaidi ya hayo ili kushinda uchaguzi ujao wa 2024.

Tatizo jingine la kiuongozi kwa mkuu huyo ni umri, wakati Amerika na mataifa ya Ulaya yanaikemea Afrika kwa kuwa na viongozi wazee na kupiga vita baadhi yao kuwa walitakiwa kupumzika na kutafuna pensheni au mafao uzeeni, safari hii suala la umri wa Rais Joseph au Joe Biden, anayetamani muhula mwingine wa urais, linaanza kuzozaniwa.

Mfano baadhi ya Waamerika wanaanza kusema kuwa babu huyo wa miaka 80, ikiwa atataka tena urais anahatarisha hatima yake na kwamba anamfagilia njia Donald Trump.

Kura za maoni sasa zinaonyesha kuwa wengi wanaamini kuwa Rais Joe Biden asigombee tena kutokana na umri wake. Ingawa wapo wanaoamini amefanya kazi nzuri kiasi , mfano kuanzia kuimarisha Umoja wa Kujihami NATO hadi kuisaidia Ukraine kupambana na mvamizi Urusi.

Watu wanahisi kampeni yake haitakuwa na shauku wala kusisimua kwa sababu ni mzee sana. Uwezo wa kiakili wa Biden na wa mwili wanaona kuwa nao umepungua na kuna uwezekano hatamaliza muhula wa pili lakini wapiga kura wana wasiwasi zaidi na Makamu wa Rais Kamala Harris, kuwa kazi hiyo pengine itamuwia ngumu.

Baadhi wanaona kuwa ni uongo kudai eti Democrat haina watiania wanaofaa, wakimtaja Gavana Gretchen Whitmer, Gavin Newsom, Roy Cooper au Wes Moore.

Wagombea hawa wanapaswa kuonyesha uhodari wa kisiasa na kusonga mbele na kuachana na kukirudisha chama nyuma ambacho huenda kikawanyima wapiga kura vijana haki yao.

Wanaomfuatilia kwenye nyendo za urais wanamwona Biden kuwa anafanya kama Trump kwa kuweka maslahi yake binafsi mbele badala ya yale ya nchi.

Isipokuwa mambo yatabadilika, dunia itakuwa ikishikilia pumzi yake kila wakati Biden anapotembea kwenye jukwaa au kuhutubia umati.

Anaweza kuingia kwenye historia kama mtu aliyewaokoa Waamerika kutoka kwa Trump mwaka 2020, ila akasababisha kumrejesha ofisini kwa mara nyingine Novemba 2024 japo naye ni mkongwe akiwa na miaka 77, Rais akimzidi na mitatu.

Rais Joe Biden, anaelezwa kuwa anakosa utaalamu wa kimikakati, tena anaonywa kuishauri Israel jinsi ya kupigana vita dhidi ya Hamas, linaripoti gazeti la The Philadelphia Inquirer.

Dunia ilitazama mzozo huo mnamo 2021 wakati Biden alipoamuru kuondolewa wanajeshi wa Marekani huko Afghanistan.

Suala la Israeli na Hamasa , linampa mtihani kwenye kampeni za uchaguzi kama gazeti la The Philadelphia Inquirer.

linavyosema:"Kusitisha" vita kwa madhumuni ya kufanikisha misaada ya kibinadamu hakufai kuwa wito wa Biden kwa Isarel.

Hamas hawawezi kuaminiwa. Kuacha mapigano katika hatua hii kutaipa Hamas muda wa kujipanga upya na inaweza kuwa na madhara kwa Israel kushinda vita hivyo. Mapambano dhidi ya Hamas yanapaswa kuendelea hadi mwisho.

Lakini pia wengine wanachukulia kushindwa kumdhibiti Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu kwenye vita yake na Hamas kuwa ni udhaifu wa Rais Biden.

Philladephia linaandika tena kuwa kuwezesha kulipiza kisasi kwa umwagaji damu, unaofanywa na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, ambaye pia ana tuhuma za ufisadi, kumemgharimu Joe Biden kura za baadhi ya watu.

Gazeti linasema dunia haiwezi kusimama tu na kushuhudia vifo na mauaji ya kutisha ya maelfu ya Wapalestina. Matukio waliyofanyiwa Israel hayaikingi na ukosoaji wa unyama inaoufanya kwa Wapalestina tena kwa kuungwa mkono kwa maneno na silaha kutoka Marekani.

Huenda wengine wasimpigie kura kiongozi huyo wanayemtazama kuwa anaangalia mauaji haya na asifanye chochote kuyakomesha.

Msumari mwingine kwenye kichwa wa urais wa Marekani 2024 unahoji uwezekano wa kuchaguliwa tena kwa Donald Trump kuwa rais.

Gazeti hilo linaandika maoni ya baadhi ya wasomaji likisema kwa wale wanaounga mkono na kusema watampigia kura Trump, ni wakati wa kuamka na kubadilika.

Linaongeza kuwa kuchaguliwa tena kwa Trump kutamaanisha kuanguka kwa demokrasia ya taifa hilo na mwanzo wa ubabe, au Amerika mbaya zaidi.

Je, huu ndiyo urithi tunaotaka kuwaachia watoto na wajukuu zetu? Kwa hakika, kuna wasiwasi na umri wa Joe Biden lakini ni vyema kufikiria njia mbadala. Ushauri wa msomaji huyo kwa wale ambao hawaogopi urais wa pili wa Trump ni huu "ogopa, ogopa sana."



## Chuo chazindua dawati la jinsia kupinga ukatili

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida limezindua rasmi dawati la jinsia katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA), Kampasi ya Singida kwa lengo la kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi wa taasisi hiyo.

Mkuu wa Dawati la Jinsia wa Jeshi la Polisi mkoani hapa, Mkaguzi wa Polisi, Amina Abdallah, akizungumza jana kwenye uzinduzi huo alisema dawati hilo litasaidia wanafunzi wanaopata na matatizo ya kunyanyaswa kutoa taarifa ili changamoto zao zifanyiwe kazi.

Alisema viongozi wa dawati hilo watakuwa wanapokea taarifa kabla ya kuzifikisha ngazi za juu na kuwataka wazingatie suala la usiri ili wanafunzi waweze kuwa na imani na dawati hilo.

Aidha, alipongeza uongozi wa taasisi hiyo kwa kazi nzuri ambayo imesaidia kudhibiti vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia katika msimu wa masomo uliopita hakujaripotiwa matukio ya unyanyasaji wa kijinsia yakiwamo ya ubakaji na ulawiti ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

"Huu utaratibu wa kuwa na dawati la kijinsia usiishie katika taasisi hii bali uenezwe katika vyuo vingine na shule za msingi kwa kutoa elimu ya kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia na hiyo ndio itakuwa njia nzuri ya kukabiliana na matukio hayo," alisema.

Katika kuhakikisha dawati hilo linapata nguvu kushughulikia kero za unyanyasaji wa kijnsia kwa wanafunzi walichaguliwa wajumbe watatu kusimamia ambao ni Waziri wa Afya kutoka Serikali ya Wanafunzi ya taasisi hiyo, Ramla Mchomvu, Mkutubi Francis Majele na Mlezi wa wanafunzi, Asia Hansy.

Makamu Mkuu wa Taasisi hiyo, Flora Lemnge, aliwataka wanafunzi hao watakapokuwa na changamoto yoyote ya ukatili wa kijinsia kwenda kutoa taarifa kwa wajumbe hao ambao ni wasiri na wana uzoefu mkubwa na kwa wavulana aliwataka kwenda kumwona Mkutubi Majele.

"Dawati la jinsia linasaidia kuweka mazingira bora kwa wanafunzi na kama wataweza kuongea na kupata sehemu ya kusema madhira yao walioyapata kwa ukaribu tena kwa mtu ambaye amemzoea ni jambo jema sana," alisema.

Alisema katika kampasi hiyo wamechaguliwa baadhi ya walimu na watumishi kuwa wajumbe wa dawati hilo ambao watasaidia kupokea taarifa kutoka kwa waathirika na kuzifanyia kazi na kuyafikia malengo ya kutokomeza ukatili katika taasisi hiyo na nchi kwa ujumla.

Mwanafunzi wa taasisi hiyo Pendo Maube, akizungumza kwa niaba ya wenzake alisema kupitia uzinduzi huo wamejua fursa mbalimbali ambazo zinapatikana katika dawati hilo la kijinsia ikiwamo haki zao na namna ya utoaji wa taarifa pale panapotokea tatizo la ukatili wa kijinsia.

Katika uzinduzi huo elimu mbalimbali zilitolewa na Mkaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Singida, Mwantumu Bakari, akiongozana na wataalamu wa jeshi hilo walitoa mafunzo ya kukabiliana na majanga ya moto.

# Msajili Hazina kuimarisha kampuni zitengeneze faida

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, amesema serikali inaendelea kuimarisha kampuni zote ambazo zinaubia nazo ili kuziwesha kuanza kutengeneza faida na kuziondoa kwenye hali ya kujiendesha kwa hasara.

Alisema hayo jana, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutia saini makubalianao baina ya serikali na wanahisa wa Kampuni ya Mbeya Cement.

Alisema, hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuitaka ofisi yake kusaidia kuimarisha uwezo wa kampuni zenye ubia na serikali ili kuongeza tija na kuzalisha faida.

"Leo kama mnavyoshuhudia wanahabari tumetiliana saini ya makubaliano katika mambo mbalimbali ambayo sisi kama serikali na wanahisa wengine tulipaswa kuyafanyia kazi ili kampuni hii ya Mbeya Cement kuanza uzalishaji na kuzalisha faida," alisema Mchechu.

Alisema moja ya mambo ambayo serikali ilipaswa kufanya ni kufuta deni la Sh. bilioni 170 la kampuni hiyo, lakini kurejesha leseni za uchimbaji.

"Mambo ambayo sisi serikali tulipaswa kufanya tumefanya ili kuongeza ufanisi katika kampuni hii ambayo ilikuwa inategemewa sana kwenye bidhaa ya saruji katika mikoa ya kusini hata nje ya nchi kama DR Congo, Zambia, lakini mikoa ya Kigoma, Katavi, Songwe na Ruvuma," alisema.

Kadhalika, alisema sehemu ya makubaliano hayo ni Bodi ya Kampuni hiyo kuundwa upya na mwenyekiti wake atakuwa anateuliwa na serikali.

"Pia tumekubaliana kupitia upya katiba na waraka wa wanahisa, hii yote ni katika kuongeza ufanisi ambao ulikosekana awali na kufanya kampuni hii kujiendesha kwa hasara, sasa itaanza kurekodi faida baada ya mabadiliko haya na kukubaliana haya tuliyosaini leo," alisema.

Kadhalika, kutokana na makubaliano ambayo yamewezesha kufanyiwa kazi kwa kero zote, wananchi wategemee kampuni hiyo kuanza uzalishaji wa saruji ya Tembo Cement, ambayo ilikuwa kipenzi cha Watanzania.

Mmoja wa wanahisa wa kampuni hiyo, Rajesh Surana, ambaye ni Meneja wa Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Kampuni ya HOLCIM GROUP, alisema wanaishukuru serikali kwa kuharakisha mabadiliko hayo.

"Tunaishukuru sana Serikali ya Tanzania kupitia Msajili wa Hazina kwa kuharakisha mabadiliko haya sasa tunaangalia mbele katika kutoa huduma bora kwa wateja wetu na kuzalisha faida," alisema Surana.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akiagana na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mati Super Brands Ltd ya mjini Babati mkoani Manyara, David Mulokozi baada ya mazungumzo, mjini Dodoma juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC akemea rushwa utoaji huduma kwa wananchi

**Na Renatha Msungu,** MPWAPWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amekemea vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya viongozi wa kata na vijiji katika utoaji huduma za kijamii kwa wananchi.

Senyamule, alisema hayo juzi wakati wa ziara yake kijiji cha Kinusi, Kata ya Ipera, wilayani Mpwapwa kwa ajili ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Alisema, watendaji wanapaswa kutoa huduma bure kwa wananchi sio kuwatoza fedha kama baadhi ya viongozi wanavyofanya na kusisitiza atakayebainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

"Naomba muache kuwatoza wananchi fedha za utoaji huduma wanazohitaji, mnapaswa kuwatumikia kama sheria ya kazi inavyowaelekeza," alisema Senyamule.

Akijibu kero mbalimbali zilizowasilishwa mbele yake, alikemea rushwa kwa viongozi wa kata na vijiji kwa kuwa huduma bure ni haki ya mwananchi yeyote.

"Hakuna mwananchi kuombwa fedha kwa ajili ya kupatiwa huduma kwa mtendaji wa kijiji kwani huko ni kuichafua serikali," alisema Senyamule.

Alisema serikali inawalipa mishahara viongozi na posho kwa ajili ya matumizi yao ya ziada kila mwezi na haya yote yamefanywa ili wananchi wapate huduma bure.

Senyamule amesisitiza mambo kadhaa kwa watendaji wa Halmashauri ya Mpwapwa ikiwa ni pamoja na viongozi wa vijiji kufanya vikao.

Pia alisisitiza wananchi, wazazi na walezi kuhakikisha watoto waliofikia umri wa kuanza shule wanaandikishwa.

Alisisitiza utunzaji wa mazingira kwa wakazi wa Kata ya Ipera na viongozi wa vijiji kusimamia kampeni ya kupanda miti mitano kwenye kila kaya ili kuzuia athari za mmomonyoko wa udongo na kuikijanisha Dodoma.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Sophia Kizigo, aliwataka wananchi kusimamia na kuilinda miradi inayoanzishwa kwenye maeneo yao kwa kuwa ina manufaa kwao itakapokamilika.

"Tusimamie miradi inayoanzishwa kwenye maeneo yetu ikiwamo ujenzi wa kituo hiki cha afya cha Ipera maana ni cha wananchi, tukisimamie ili kijengwe kwa ubora kwa kuhakikisha tunalinda vifaa vya ujenzi visiibiwe," alisema Kizigo.





# TBS yatoa mafunzo usindikaji wajasiriamali mboga, matunda

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

SHIRIKA la Viwango nchini (TBS), limeanza kutoa mafunzo maalumu kwa wajasiriamali wanaosindika bidhaa za mboga na matunda mkoani hapa ili wawe na ujuzi wa kuzalisha bidhaa zenye viwango vinavyokidhi mahitaji ya soko na kimataifa.

Mafunzo hayo yalianza juzi kwa kuwashirikisha wasindikaji zaidi ya 70 wa bidhaa hizo wanaofanya shughuli zao jijini hapa ambao pia wanafundishwa usindikaji bora wa bidhaa za kuoka.

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Noor Meghji, alisema wanatoa mafunzo hayo kwa kushirikiana na Shirika la Kusimamia Viwanda Vidogo (SIDO) na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) upande wa afya.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa kuhusu viwango vya ubora wa bidhaa wanazosindika ili kuongeza pato la wazalishaji pamoja na taifa kwa ujumla.

"Baada ya mafunzo haya ya nadharia ambayo yatadumu kwa siku tatu, washiriki watakaokuwa tayari watapata fursa ya kutembelewa na maofisa wetu ili kupata mafunzo zaidi ya vitendo pamoja na ushauri kuhusu usindikaji," alisema Noor.

Alisema mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwa wasindikaji nchini na kuwataka kujitokeza na kufuatilia kwa umakini mafunzo hayo ili wazalishe bidhaa zenye viwango.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amina Nalicho, aliwataka wasindikaji wa bidhaa za chakula katika jiji hilo kuboresha mazingira wanayofanyia kazi kwa kuyafanya yawe safi ili zisiwadhuru walaji na kupoteza soko lao.

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia wasindikaji hao kuongeza ubora wa bidhaa hizo na kufikia viwango ambavyo vinakubalika kwenye soko.

Vilevile, aliwataka wakulima kuepuka kutumia sumu kwenye mazao kwasababu ubora wa mazao hushuka na wakati mwingine kuwadhuru walaji.

"Kuna ule utaratibu wakulima wengi wanautumia, mkulima wa mahindi anatenga gunia kadhaa kwa ajili ya kula yeye na familia yake anahifadhi kwenye mifuko ya kinga njaa halafu ya kuuza anaweka sumu ya kuzuia wadudu, naomba tuache utaratibu huo kwa sababu tunaweza kudhuru ndugu zetu," alisema Amina.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwapongeza maofisa wa TBS kwa kuanzisha mafunzo hayo ambayo yatawasaidia wasindikaji kuongeza ujuzi.

Aliwaomba maofisa hao kuendelea kutoa mafunzo hayo kwa wazalishaji wengine ili elimu hiyo isambae zaidi na uzalishaji wa bidhaa uwe na viwango vinavyostahili kwa binadamu.

Alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa inayozalisha kwa kiasi kikubwa matunda na mboga na kwamba wasindikaji lazima wapate mafunzo ili wasindike vizuri na kuuza kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi.

Pia Jiji la Mbeya lina faida ya kuwa na kiwanda cha kusindika mboga na matunda ambacho kimejengwa kupitia programu ya uboreshaji wa mnyororo wa Thamani wa Kahawa, Chai, Mboga na matunda ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT.



Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki (wa pili kulia), akikabidhi msaada wa magodoro kwa ajili ya kulalia wafungwa kwa Mkuu wa Gereza la Iringa, SSP Daniel Mwakapili katika gereza hilo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Shule 57 zapewa vyandarua na MSD kudhibiti malaria

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BOHARI ya Dawa (MSD) Mkoa wa Iringa imekabidhi zaidi ya vyandarua 18,000 kwa shule za msingi 57 katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kupunguza maambukizi ya ugonjwa wa malaria nchini.

Meneja wa MSD Mkoa wa Iringa, Robert Lugembe, akiongoza usambazaji huo katika Shule ya Msingi Lunguya, alisema vyandarua hivyo vitagawiwa kwa watoto wapatao 18,774.

"Tumekuja Mkoa wa Njombe, tupo katika wilaya mbili ambazo tutasambaza vyandarua hivi, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa na kila mtoto atapata chandarua chake na ataenda nacho nyumbani kwa ajili ya matumizi," alisema Lugembe.

Mratibu wa Malaria Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Suleiman Zamilisi, alisema bado kuna changamoto ya ugonjwa wa malaria na kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya wakazi 690 waliugua malaria, kati yao watoto 118 walikuwa ni waathirika wa ugonjwa huo.

"Sasa katika mapambano ya ugonjwa huo, halmashauri inatekeleza mpango wa kupambana na ugonjwa wa malaria," alisema Zamilisi.

Katibu Tawala Wilaya ya Njombe, Agatha Mhaiki, aliwataka viongozi wa idara ya afya katika vijiji kuendelea kutoa elimu kwa wazazi na walezi ili kutumia vizuri vyandarua hivyo ambavyo vipo salama kwa afya ya binadamu.

"Hakikisheni wazazi wanajua umuhimu wa kutumia vyandarua muwaambie wasifugie kuku wala kufunikia mboga wala kupelekwa kama neti za uvuvi, lakini tukipita huko barabarani kuna vifuu, kuna madimbwi, nyumbani kuna majani marefu huko ndio mbu wanapokaa na kuzaliana," alisema Mhaiki.

Alisema serikali imeweka mpango madhubuti ya kudhibiti na kuenea kwa ugonjwa wa malaria kwa kuhakikisha kuwa wananchi wanapata vyandarua kwa asilimia 80 hadi kufikia mwaka 2030.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Christopher Sanga, alisema vyandarua hivyo vitasaidia kupunguza au kumaliza kabisa ugonjwa huo, kwa sababu hivi sasa halmashauri imefanikiwa kupunguza ugonjwa wa malaria kutoka asilimia 4.6 mwaka 2020 hadi asilimia 2.3 Juni 2023.

# TANAPA yawapa magodoro wafungwa Gereza Kuu Iringa

**Na Nebart Msokwa,**
IRINGA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) limetoa msaada wa magodoro 41 kwenye Gereza Kuu la Iringa kwa ajili ya wafungwa wanaotumikia vifungo mbalimbali ili kupunguza tatizo la upungufu wa vifaa hivyo kwenye gereza hilo.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, alikabidhi msaada huo juzi.

Alisema msaada huo ni sehemu ya faida ambayo hifadhi hiyo inarejesha kwa jamii.

Kadhalika, hifadhi hiyo kwa muda mrefu ilikuwa inashughulika na uchangiaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi lakini kwa sasa waliamua kutoa msaada kwenye gereza hilo ili kuwasaidia wafungwa.

Alisema ni mwendelezo wa ushirikiano kati ya hifadhi hiyo na jamii huku akisisitiza kuwa hifadhi hiyo inawathamini wafungwa kwa kuamini kuwa watu walioko gerezani wanajifunza. "Mchango huu ni sehemu ya faida tunazopata kutokana na utalii, tumekuwa tukishiriki kwenye mambo mengi, lakini hili la kuchangia gereza tumeona ni muhimu zaidi kwa wakati huu," alisema Ole Meing'ataki.

Alisisitiza kuwa wataendelea kutoa misaada mingine kwenye maeneo mengine ikiwamo kuchangia shughuli za maendeleo kama ujenzi wa vituo vya afya na elimu.

Mkuu wa Gereza la Iringa, Mrakibu Mwandamizi wa Magereza, Daniel Mwakapila, aliwashukuru maofisa wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa msaada huo na kuwa walikuwa wanakabiliwa na upungufu mkubwa wa vifaa hivyo.

Hata hivyo, alisema TANAPA ni miongoni mwa wadau muhimu ambao huwamekuwa wakiwapatia ushirikiano wanapotaka kitu chochote cha maendeleo.

"Japokuwa msaada huu haumalizi kabisa tatizo lakini mmetusaidia kwa kiasi kikubwa sana, tunaomba mwendelee kutupatia ushirikiano huu ambao tumeanza muda mrefu," alisema Mwakapila.



# NMB yatia saini makubaliano miradi maendeleo na ZPPP

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BENKI ya NMB imetia saini makubaliano ya ushirikiano na idara ya mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi (ZPPP) kwa ajili ya uendeshaji wa miradi ya maendeleo.

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini huo uliofanyika mjini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema Serikali ya Zanzibar inathamini jitihada zinazotolewa na taasisi za kifedha ikiwamo benki ya NMB katika kuwaletea maendeleo wananchi wa visiwa hivyo.

Alisema malengo ya serikali ni kuona wananchi wa chini wananufaika na fursa za maendeleo hasa kuwezeshwa katika elimu ya ujasiriamali na mikopo ili kujikwamua na hali ya umasikini.

Waziri Soraga, alisema uamuzi wa benki hiyo kuingia makubaliano na taasisi ya ZPPP inawanufaisha wananchi na miradi iliyoanzishwa na taasisi hiyo.

Ofisa Mkuu wa fedha kutoka NMB, Juma Kimori, alisema kunahitajika kuwa na ushirikiano, ni msisitizo kutoka kwa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wa kukuza uchumi wa nchi kwa sababu sekta binafsi ina nafasi kubwa katika kuchangia maendeleo ya uchumi duniani.

"Sisi kama NMB ambayo ni benki inayoongoza Tanzania tunafarajika sana kuona haya mabadiliko chanya yanayotokea ambayo tunaamini yanakwenda kuleta mapinduzi katika ukuaji wa uchumi na kuwafikia wananchi wa kawaida," alisema.

Alisema makubaliano hayo ni hatua ya uwekezaji na uwezeshaji ambao unafanyika kwa nia madhubuti ya serikali na utaendelea kuwa endelevu ili wananchi wafaidike.

Alisema NMB ni benki inayosaidia serikali kusonga mbele kukuza uchumi na hiyo sio mara ya kwanza kusaini mikataba kama hiyo ya ushirikiano na wanafarajika kuona miradi ya maendeleo inaendelea vizuri.

"Kwa Zanzibar kama sisi NMB tuna matawi manne, lakini tunaendelea kuwekeza katika mifumo na mawakala ili kuhakikisha huduma za fedha zinawafikia wananchi kwa urahisi," alisema.

Alisema benki hiyo inatambua umuhimu wa kuona uchumi wa Zanzibar unaimarika na ndiyo maana benki hiyo ikitoa elimu ya matumizi ya kidijitali na kusimamia biashara zao kwa makini na kuwa endelevu na wameshawafikia wajasiriamali 10,000 kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali na kifedha.

Kamishna wa idara ya mashirikiano baina ya serikali na sekta binafsi (ZPPP), Dk. Bili Kiwia, alisema makubaliano hayo yanaenda kutoa fursa ya mafanikio kwa wananchi wa chini hasa wajasiriamali kunufaika na miradi ya maendeleo ya taasisi hiyo.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na Ujumbe wa Umoja wa Ulaya ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Masuala ya Bahari na Uvuvi wa umoja huo, Charlina Vitcheva (wa nne kushoto), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Zaidi ya watalii 100 waingia Pemba kufungua uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATALII 168 wamefika kisiwani Pemba juzi kwa meli kubwa ya kitalii na kupokewa katika Bandari ya Mkoani ikiwa ni juhudi za kukifunguwa kisiwa hicho kiuchumi na uwekezaji.

Watalii hao walipokewa na Ofisa Mdhamini Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba, Zuhura Mgeni Othman, ambaye alisema hiyo ni miongoni mwa fursa za juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukitangaza kisiwa cha Pemba na duniani.

Alisema watalii hao wanatoka katika nchi mbalimbali za Ulaya na Marekani na walipowasili walitembelea maeneo ya vivutio vya utalii ikiwamo makumbusho.

Alisema Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa upande wa Pemba, imejikita zaidi kuwavutia watalii kutembelea majengo ya kale ambayo yamebeba historia kubwa kupitia tawala mbalimbali Zanzibar.

Vile vile, wageni hao walitembelea na kujionea vivutio vya mazao ya kilimo na viungo ikiwamo mashamba ya mikarafuu zao ambalo linastawi kwa wingi Zanzibar pamoja na vanila na pilipili manga.

"Watalii wetu walitembelea maeneo mbalimbali ambayo ni majengo ya kale yaliyobeba historia kupitia watawala waliotawala Zanzibar pamoja na mazao ya kilimo ambayo hayapatikani sehemu nyingine," alisema.

Watalii hao walisema watapata fursa ya kutembea na kujifunza vitu mbalimbali ambavyo vinapatikana kisiwani humo na vinasifika duniani kote likiwamo zao la karafuu.

**"Watalii wetu walitembelea maeneo mbalimbali ambayo ni majengo ya kale yaliyobeba historia kupitia watawala waliotawala Zanzibar pamoja na mazao ya kilimo ambayo hayapatikani sehemu nyingine," alisema.**

# Mwinyi azishukuru WB, EU ushirikano Serikali Australia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameshukuru ushirikiano wa karibu uliopo baina ya Tanzania hususani Zanzibar, na Benki ya Dunia (WB), Umoja wa Ulaya (EU) na ushirikiano wa diplomasia uliopo baina ya Australia na Tanzania.

Dk. Mwinyi alitoa shukurani hizo Ikulu, mjini hapa alipozungumza na wageni hao walioambatana na ujumbe waliofuatana nao kwa nyakati tofauti.

Alisema, taasisi hizo zina mchango mkubwa wa maendeleo ya Zanzibar hasa kukuza sekta ya afya nchini, Elimu, Utalii na Uchumi wa Buluu.

Akizungumza na Balozi wa Australia nchini Tanzania, Luke William, aliyefika kumuaga, Rais Dk. Mwinyi alipongeza ushirikino mkubwa uliopo baina ya Tanzanzia na nchi hiyo na kumueleza Zanzibar inavyonufaika na sekta ya uvuvi na mwani uliowaneemesha kinamama wengi na vijana kwa kuwa asilimia 90 ya wakulima wake ni wanawake.

Pia, Rais Dk. Mwinyi alimweleza balozi huyo azma ya kuendeleza ushirikiano uliopo baina ya Australia na Zanzibar hasa kwenye masuala ya uwekezaji, biashara na utalii.

Akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa masuala ya Bahari na Uvuvi wa Umoja wa Ulaya (EU), Charlina Vitcheva, alimweleza kuwa Zanzibar ni kisiwa kilichozungukwa na Bahari ya Hindi, inajivunia fursa nyingi zinazotokana na rasilimali bahari kwa kujikita zaidi kwenye uchumi wa buluu na utalii.

Alisema uchumii wa buluu ni sekta muhimu kwa uchumi wa visiwa hivyo na kuongeza kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inafanya kila iwezavyo kunufaika na fursa zinazotokana na sekta hiyo kwa ajili ya uchumi wa watu wake.

Aidha, alimtaka mkurugenzi kuimarisha zaidi ushirikiano wao kwenye sekta hiyo ili kujenga weledi kutokana na idadi kubwa ya Wazanzibari kujikita zaidi na masuala ya uvuvi na ajira zinazotokana na bahari.

Mwinyi alisema, serikali inawaunga mkono wavuvi na wakulima wa mwani nchini kwa kuwa imewawezesha kwa mitaji na vifaa pamoja na kuiunga mkono sekta ya utalii.

Ugeni huo ulisema utaendelea kuiunga mkono Zanzibar na Tanzania hasa kwenye masuala ya kuendeleza ushirikiano wao wa kidiplomasia na kuona fusra za uwekezaji na uchumi zilizomo Tanzania vina nufaisha pande zote na ushirikiano wao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**CATHERINE JEREMIA MZIRAY** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S4554-0019,kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **HENRY GOGARTY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: AR/RB/16417/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER JERE LEMUNGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CORONA** yenye usajili namba **T685 AYY** na CHASSIS NAMBA: **NOAT2110059047.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/6415/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF MWANGA**
**AT MWANGA**

**MATRIMONIALS CAUSE 4 OF 2023**

**WILFRED PETER SAMWEL......................PETITIONER**

**VERSUS**

**NEEMA HENDRY JOHN.......................RESPONDENT**

**TO NEEMA HENDRY JOHN**
**DAR ES SALAAM**

**NOTICE OF MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for necessary mention on 16th day of November, 2023 8:00AM before **Hon A.S.HAYATA –RM.** YOU ARE required to appear in this court without fail and you must reply petition of divorcer filed before this court within 21 days after this citation on Newspaper.

**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT** this 25th day of October,2023

DISTRICT COURT MWANGA

..................................
RESIDENT MAGISTRATE
MWANGA

Resident Magistrate
Mwanga

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SARAH CHARLES NYAHONGO** anatangaza kupotelewa na **kadi ya gari yenye namba za usajili T 318 CRW** aina ya **NISSAN MURANO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/6459/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ALLEN ROBERT MASIMBA** anatangaza kupotea kwa vyeti, cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index **No.S0806-0082** kilichotolewa na baraza la Mitihani laTarifa kupitia **CITY SECONDARY SCHOOL** mwaka **2003,** Cheti cha chuo chenye **No. 027527** Medical Training Centre - MVUMI mwaka 2010.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/318874/2022.**


***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701***

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.**

**Mob: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda, DRC zatakiwa kuondoa majeshi mpakani

**WASHINGTON,** Marekani

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ametoa wito kwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Félix Tshisekedi na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, kuondoa wanajeshi kwenye maeneo ya mpakani.

Kwa mjibu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, akielekea Japan kutoka kwa ziara yake ya hivi punde Mashariki ya Kati, Blinken alizungumza na viongozi hao kwa nyakati tofauti juu ya mgogoro katika mpaka kati ya mataifa hayo mawili na kuzitaka pande zote kupunguza mvutano baina yao.

Inaelezwa kuwa Rwanda na DRC zinashutumiana kwa uungaji mkono wa makundi ya waasi.

Msemaji wa wizara hiyo, Matthew Miller, alisema hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa kuhusu mahojiano hayo ila Ofisi ya Rais wa Rwanda ilisema Rais Kagame alisisitiza uungaji mkono mkubwa wa Blinken kwa mipango inayoendelea ya kikanda inayolenga kuleta amani na utulivu kwa DRC na kanda.

Ilivyoelezwa kuwa waasi wa M23, wanaopigana mashariki mwa DRC, wamezidisha mashambulizi tangu mwezi uliopita, huku Umoja wa Mataifa (UN) ukiripoti kuwa watu wengine 200,000 wameyakimbia makazi yao.

Taarifa zilisema mapigano makali yaliendelea siku chache zilizopita, huku M23 wakichukua tena baadhi ya maeneo kilomita chache kutoka mji wa Goma, mji mkuu wa jimbo la Kivu Kaskazini, mashariki mwa DRC. **BBC**



Mafuriko yanavyoendelea kuwaathiri wakazi Somalia, ikibainishwa kuwa zaidi ya watu 113,000 wamepoteza makazi yao kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha nchini humo. **PICHA: REUTERS**

# UN: Gaza yageuka uwanja wa makaburi

**GAZA,** Palestina

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, amesema ukanda wa Gaza kwa sasa umegeuka uwanja wa makaburi ya watoto kutokana na vita vinavyoendelea, huku akieleza kuwa mgogoro huo umekuwa janga la kibinadamu katika ukanda huo.

Kwa mujibu wa taarifa ya UN iliyotolewa jana na kiongozi huyo, hali ni ya wasiwasi katika maeneo ya mjini Jerusalem, ukingo wa Magharibi na kwenye mpaka baina ya Israel na Lebanon, kutokana na vita vinavyoendelea kati ya Israel na kundi la Hamas.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Afya ya Gaza ambayo inadaiwa kuwa chini ya Hamas, idadi ya Wapalestina waliouliwa Gaza tangu kuanza kwa vita hivyo Oktoba 7, mwaka huu, imepanda hadi kufikia 10,022.

Wizara hiyo ilisema maelfu ya wanawake na vijana ni miongoni mwa wale waliouliwa katika mashambulizi ya kulipiza kisasi ya kutokea angani na ya ardhini ya Israel.

Guterres analilaani kundi la Hamas kwa vitendo vyake vya kigaidi huku akirudia wito wake kutaka zaidi ya mateka 200 ambao wamekuwa wakishikiliwa na wanamgambo hao katika ukanda wa Gaza kwa mwezi mmoja sasa, waachiwe huru mara moja.

**Wakati hayo yakiendelea, ilibainishwa kuwa kundi la Hamas limerusha roketi kuelekea Israel kutokea Lebanon. Huku tawi la kijeshi la Hamas, Al-Qassam birgades, likisema kwamba limefyatua maroketi 16.**

Pia alisema usitishwaji mapigano kuruhusu utoaji wa misaada ya kibinadamu sharti utekelezwe na Israel na watawala wa Hamas huko Gaza ili kufikisha mwisho analoliita jinamizi la vita.

Pia alisema operesheni ya ardhini ya jeshi la Israel na mashambulizi ya mabomu yanayoendelea yanawaathiri raia, hospitali, kambi za wakimbizi, misikiti, makanisa na vifaa vya Umoja wa Mataifa yakiwamo makazi.

"Hamas na wanamgambo wengine wanawatumia raia kama ngao ya binadamu kujilinda na wanaendelea kuvurumisha maroketi kiholela kuelekea Israel," alisema.

Aidha, akionyesha huzuni kubwa Guterres, alisema malori 400 ya mahitaji ya misaada yamefanikiwa kuingia ukanda wa Gaza katika kipindi cha wiki mbili zilizopita na kwamba kabla ya vita kuanza malori 500 yalikuwa yakiingia Gaza kila siku.

Aliongeza kuwa mafuta yanayohitajika kwa dharura na ambayo ni muhimu kuendeshea shughuli katika hospitali, hayakuweza kusafirishwa kufika Gaza.

**MAREKANI**

Wakati UN ikisisitiza usitishwaji wa mapigano, Marekani nayo imekiri kumetokea kwa vifo vya maelfu ya raia katika ukanda wa Gaza, ingawa haikutoa takwimu halisi.

Taarifa hiyo ilitoka baada ya Rais Joe Biden kuhoji awali juu ya uhalali wa takwimu zinazochapishwa na Wizara ya Afya ya Gaza. Huku maofisa wa UN wakieleza kuwa takwimu zinazotolewa na wizara hiyo ni dhahiri na za kuaminika.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Marekani, Pentagon, Brigedia Jeneali, Pat Ryder, alisema kuhusiana na idadi ya raia waliouliwa Gaza, wanafahamu zimefikia maelfu.

Ryder pia alisema hiyo ndio sababu kwa nini kimekuwa kipengele cha kusisitizwa na Israel na mataifa mengine katika eneo hilo kuhusu jinsi ilivyo muhimu kuruhusu msaada wa kibinadamu na misaada mingine kupelekwa Gaza.

Wakati hayo yakiendelea, ilibainishwa kuwa kundi la Hamas limerusha roketi kuelekea Israel kutokea Lebanon. Huku tawi la kijeshi la Hamas, Al-Qassam birgades, likisema kwamba limefyatua maroketi 16.

Ilielezwa kuwa mji wa Nahariyya na Haifa kuisni imeshambuliwa huku Hamas ikisema katika mtandao wa Telegram kwamba mashambulizi hayo yalifanywa kutokana na mashambulizi ya Israel dhidi ya watu wao katika Ukanda wa Gaza.

Likijibu kauli hiyo, Jeshi la Israel lilidai roketi 30 yalifyetuliwa kuelekea kaskazini mwa Israel na kusababisha ving'ora vya tahadhari ya mashambulizi ya angani kulia katika vijiji kadhaa.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa kundi la Hamas lina wapiganaji kadhaa kusini mwa Lebanon na limewahi kudai kufanya mashambulizi nchini Israel kutokea huko.

**AFRIKA KUSINI**

Kutokana na migogoro hiyo inayoendelea, serekali ya Afrika Kusini, ilisema itawaita nyumbani wanadiplomasia wake kutoka Israel, ikielezea wasiwasi wake kutokana na hali ya Gaza.

Pretoria pia ilisema nafasi ya Balozi wa Israel, nchini humo inazidi kuwa mbaya kwa siku hadi siku, ikimshutumu mwanadiplomasia huyo kutoa maoni makali kwa watu wanaoikosoa Israel.

Waziri katika Ofisi ya Rais, Khumbudzo Ntshavheni, aliuambia mkutano na wanahabari bila kutoa taarifa za kina kwamba, serikali ya Afrika Kusini imeamua kuondoa wanadiplomasia wote kutoka ubalozi wa Tel Aviv.

Pretoria, kwa kipindi kirefu imekuwa ikiunga mkono harakati za Palestina, ambako chama tawala cha (ANC) kimekuwa kikihusisha na harakati zake za kipindi cha ubaguzi wa rangi.

Vile vile, inaelezwa kuwa toka tukio la Oktoba 7, mwaka huu kundi la Hamas, kushambulia Israel, kumekuwa na mivutano ya kidiplomasia kwa wanaounga mkono ama kukosoa upande mwingine wa mgogoro wa Israel na Hamas. **DW, VOA**

# KILICHOMREJESHA TENA FEI TOTO TAIFA STARS HIKI HAPA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuonyesha kiwango kizuri kwenye mechi za hivi karibuni za Ligi Kuu Tanzania Bara, hatimaye kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', amerudishwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Fei Toto, aliyetoa pasi mbili za mwisho za mabao 'assist', akiiongoza timu yake ya Azam FC kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Mashujaa FC Jumatano iliyopita katika Uwanja wa Lake Tanganyika na kufunga moja Ijumaa iliyopita kwenye mechi ambayo Azam ilishinda 3-1 dhidi ya Ihefu FC, Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, ni mmoja kati ya wachezaji 35 walioitwa na Kocha Mkuu wa Stars, Mtunisia Adel Amrouche, kuunda kikosi kitakachoingia kambini kwa ajili ya michezo ya kusaka tiketi ya kufuzu Kombe la Dunia, dhidi ya Niger na Morocco.

Mchezaji huyo hakuwapo kwenye kikosi kilichofanikiwa kutinga AFCON dhidi ya Algeria, kitu ambacho kilipigiwa kelele na baadhi ya mashabiki wa soka.

**Mtunisia huyo ameteua makipa watano, mabeki 12, viungo tisa na mastraika tisa kuunda kikosi hicho.**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kwa upande wa makipa kocha huyo amewateua Beno Kakolanya wa Singida Fountain Gate, Aishi Manula aliyekuwa majeruhi kwa muda mrefu na kutokuwapo kwenye kikosi hicho naye anarejea tena, Aboutwalib Mshery na Metacha Mnata wote wa Yanga na Kwesi Kawawa wa Karlslunden ya Sweden.

Mabeki ni Dickson Job, Ibrahim Hamad 'Bacca', Bakari Mwamnyeto, Nickson Kibabage wote wa Yanga, Lusajo Mwaikenda na Edward Manyama (Azam FC), Haji Mnoga (Aldershot Town ya Uingereza), Abdi Banda (Richard Bay ya Afrika Kusini), Novatus Miroshi (Shakhtar Donetsk ya Ukraine), Edwin Balua (Prisons), Abdulmalik Zacharia kutoka Namungo FC na Omari Mvungi wa FC Nantes ya Ufaransa.

Wachezaji wa viungo wa kukaba, washambuliaji pamoja na mawinga ni, Ibrahim Joshua wa Tusker ya Kenya, Mzamiru Yassin (Simba), Sospeter Bajana na Fei Toto kutoka (Azam FC), Baraka Majogolo (Chippa United ya Afrika Kusini), Mudathir Yahaya (Yanga), Mourice Ibrahim (FK Spartak ya Serbia), Himid Mao (Tala'ea El Gaish ya Misri) na Ladaki Chasambi kutoka Mtibwa Sugar.

Mastraika walioitwa ni mkongwe John Bocco wa Simba ambaye amerejeshwa kwa mara nyingine tena, akiwa pamoja na Kibu Denis kutoka klabu hiyo.

Wengine ni nahodha, Mbwana Samatta (PAOK FC ya Ugiriki), Simon Msuva (JS Kabylie ya Algeria), Abdul Suleiman Sopu (Azam FC), Ben Starkie (Basford United ya Uingereza), Matteo Antony (Mtibwa Sugar), Charles M'mombwa (Macarthur ya Australia) na Clement Mzize wa Yanga.

## AFCON 2027...




Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, akizungumza na Mawaziri wa Michezo wa Tanzania, Kenya na Uganda, ambao walikutana na timu ya wataalamu kutoka nchi hizo kuweka mikakati ya pamoja kuelekea mashindano ya Fainali za Mataifa Afrika (AFCON) 2027, zitakazofanyika kwa ushirikiano wa nchi hizo. Katika kikao hicho kilichofanyika jana Mombasa nchini Kenya, mbali na Msigwa Tanzania iliwakilishwa na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, Rais wa Shirikisho la Soka, Wallace Karia, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Michezo, Ally Mayai, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa, Neema Msitha na wataalamu wengine. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kifo cha Kessy chaitikisa bendi ya Town Classic

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Town Classic, imesimamisha maonyesho yake kwa muda usiojulikana kutokana na kifo cha mmiliki wake, Patrick Kessy, aliyefariki dunia jijini Arusha juzi.

Meneja wa bendi hiyo, Andrew Sekidia, alisema kwa mshtuko walioupata wa kumpoteza bosi wao, kwa sasa wameamua kujipa muda mrefu wa maombolezo hadi hapo baadaye watakapoona inafaa kukutana.

"Inauma sana kuona mtu ambaye alikuwa anapigania kuhakikisha muziki wa dansi unarudi kwenye chati, anatoweka ghafla kiasi hiki, ni afadhali angekuwa anaumwa, lakini amefariki ghafla," alisema Sekidia.

Alifafanua kuwa Kessy alinunua vyombo vya muziki na kukusanya wanamuziki na kuanzisha bendi ya Town Classic, ameiacha ikiwa na mwaka mmoja tu na kwamba hilo ni pigo kubwa kwao.

"Pamoja na kwamba alikuwa ni mmiliki wa bendi, lakini alikuwa mwimbaji mzuri wa muziki na dansi, ndiyo maana aliamua kuwekeza kwenye muziki huu ili kuurejeshea heshima," alisema.

Aidha, Sekidia alisema mwili wa marehemu Kessy unatarajiwa kurejeshwa jijini Dar es Salaam na kuhifadhiwa katika Hospitali ya Lugalo kusubiri taratibu za maziko.

Sekidia alisema mwili huo unatarajiwa kufikishwa jana, huku shughuli za maombolezo zikiendelea nyumbani kwa marehemu eneo la Mbezi Beach Dar es Salaam.

"Familia ya Moshi mkoani Kilimanjaro na Dar es Salaam ikikamilisha ratiba ya maziko tutajulishwa, kinachoendelea sasa ni shughuli za maombolezo," alisema.

**Familia ya Moshi mkoani Kilimanjaro na Dar es Salaam ikikamilisha ratiba ya maziko tutajulishwa, kinachoendelea sasa ni shughuli za maombolezo.**

# Kongamano la Access 2023 kufanyika kesho

**Na Mwandishi Wetu**

KONGAMANO kubwa la kimataifa la muziki la Access linatarajiwa kufanyika kesho katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Kongamano hilo linatarajiwa kuhudhuriwa na wasanii na wadau wa muziki zaidi ya 2,000 kutoka katika nchi mbalimbali Afrika huku likienda sambamba na tamasha kubwa la muziki.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Dk. Kedmon Mapana, alisema serikali inashirikiana kwa karibu na Taasisi ya Music in Africa wanaoendesha kongamano hilo.

Alisema kongamano hilo linatarajiwa kuhusisha wasanii, waandaaji wa muziki, wamiliki wa lebo na wadau wa muziki.

Aliongeza kongamano hilo linafanyika nchini kwa mara ya pili, ambapo lengo lake ni kuhakikisha linawaweka wasanii na wadau mbalimbali pamoja katika kuhakikisha wanafikia malengo ikiwamo kuuza kazi zao katika mitandao na nje ya nchi.

"Serikali chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kushirikiana na Taasisi ya Music in Africa, tumeandaa kongamano la wasanii litakaloambatana na burudani, lengo ni kuwapa wasaa wetu fursa ya kujifunza na kujitangaza zaidi kimataifa," alisema Dk. Mapana.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Taasisi ya Music in Africa, Eddie Hatitye, alisema kongamano hilo litahusisha wadau wakubwa na kuwakusanya pamoja wasanii mbalimbali kutoka Afrika.

Alisema kongamano hilo litasaidia wasanii kutengeneza mahusiano ya karibu na wadau mbalimbali wa muziki ili kunufaika na kazi wanazozifanya kila siku.

Hatitye alisema baada ya kongamano hilo, kutafanyika tamasha kubwa la muziki ambapo wasanii mbalimbali watapanda jukwaani kuimba.

"Kongamano pia litahusisha wasanii wa muziki wa singeli kwa mara ya kwanza mwaka huu kutokana na kuwa na mashabiki wengi, lengo ni kutengeneza mahusiano mazuri baina ya wasanii na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubadilishana mawazo, kupata elimu na kufanya biashara kwa pamoja," alisema Hatitye.

Alisema baadhi ya wasanii watakaopanda jukwaani ni pamoja na Christian Bella, Mario, Sho Madjozi na wengineo kutoka nchi mbalimbali.

Tamasha hilo linatimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake na limeshafanyika katika nchi za Afrika Kusini, Ghana, Kenya na Tanzania linafanyika kwa mara ya pili mfululizo.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### CHERKI AFUATILIWA UNITED

KLABU za Manchester United na Newcastle United zote zinamfuatilia mshambuliaji wa Lyon, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 20, ambaye mkataba wake unamalizika Juni 2025. ***(Football Insider)***

#### FERNANDES ALENGWA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Ureno, Bruno Fernandes, 29, anatarajiwa kulengwa na Klabu za Saudi Arabia Januari. ***(Rudy Galetti)***

#### MOYES NA WEST HAM

KOCHA wa West Ham, David Moyes, 60, hayuko katika hatari ya kutimuliwa licha ya timu yake kushinda mchezo mmoja tu kati ya saba zilizopita za Ligi Kuu England, lakini kocha huyo huenda asiongezwe mkataba wake ambao unamalizika msimu ujao wa majira ya joto.***(Talksport)***

#### RABIOT MKATABA MREFU

KLABU ya Juventus inaimani kwamba watakubaliana kuhusu mkataba mpya wa muda mrefu na kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot, 28, ambaye alisaini nyongeza ya mwaka mmoja wakati wa majira ya joto. ***(90 Min)***

#### WIRTZ AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City ina nia ya muda mrefu ya kumnunua kiungo wa kati wa Ujerumani, Florian Wirtz, 20, na walimtazama mchezaji huyo wakati timu yake ya Bayer Leverkusen ikiichapa Hoffenheim Jumamosi. ***(90 Min)***

#### BOTELI AMULIKWA JUVE

KLABU za Juventus na Everton zote zinamfuatilia mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach mwenye umri wa miaka 17, Winsley Boteli. ***(Fabrizio Romano)***

#### KONATE AITAJA PSG

MLINZI wa Liverpool, Ibrahima Konate, 24, amekiri kwamba amekuwa na ndoto ya kuichezea Paris St-Germain, lakini kuhamia kwa mabingwa hao wa Ligue 1 si mojawapo ya "lengo" la sasa. ***(Canal Plus, Goal)***

#### ETTIFAQ KUIMARISHA KIKOSI

KOCHA wa Al-Ettifaq, Steven Gerrard, amesema "atazunguka Ulaya" kwa ajili ya kulenga wachezaji zaidi wakati wa uhamisho huku akipania kuimarisha kikosi chake Januari. ***(Mail)***

#### BELLINGHAM ATAJWA

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard, amesema bodi ya klabu hiyo ilimnyima nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa England na Real Madrid, Jude Bellingham, 20, alipokuwa Birmingham City. ***(Obi One)***

#### MANNING KUTUA BRISTOL

KOCHA wa Oxford United, Liam Manning anakaribia kuwa kocha mpya wa Bristol City. ***(Sky Sports)***

#### TCHOUAMENI HATARUHUSIWA

REAL Madrid 'hawana nia' ya kumruhusu kiungo wa Ufaransa, Aurelien Tchouameni, 23, kuondoka katika klabu hiyo huku Arsenal na Liverpool wakimtaka mchezaji huyo. ***(90 Min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTINO AFUNGUA RASMI MLANGO WA KUREJEA SPURS

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Mauricio Pochettino, amedokeza kwamba hata kama mashabiki wa Tottenham Hotspur wangemzomea haimfanyi ashindwe kurejea katika klabu hiyo siku zijazo.

**Pochettino, alifutwa kazi na Spurs Novemba 2019 - miezi michache tu baada ya kuiongoza klabu hiyo kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza alicheza dhidi ya timu yake hiyo ya zamani kwa mara ya kwanza Jumatatu usiku akiwa na Chlesea kwenye Uwanja wa Tottenham Hotspur. Chelsea ilishinda mabao 4-1.**

Sasa akiwa msimamizi wa mpinzani wa ndani, Muargentina huyo alikiri kwamba "viungo vyake vya kihisia" na "hisia" za Tottenham bado anazo ikiwa ni miaka minne tangu atimuliwe, na hata mapokezi ya chuki yasingemzuia kufanya kazi tena katika klabu.

"Ndiyo, uhusiano wetu ulivunjika nilipomaliza mkataba wangu," alisema Pochettino.

"Lakini tunazungumza juu ya uhusiano wa mhemko na hisia, na hiyo haijavunjwa. Haitavunjika ikiwa wangenipigia kelele. Haitabadilisha historia yangu, maisha yangu ya zamani. Ni kitu ambacho kitakuwa na wewe kila wakati."

Kuhusu kurejea Spurs, Pochettino aliongeza: "Nani anajua? Ni kama maisha, huwezi jua kitakachotokea kesho. Tunahitaji kufurahia leo. Nafikiri sasa niko na miaka 51, ninafikiria zaidi kuhusu hilo na kufurahia leo na kutotazama sana siku zijazo, kwa muda mrefu. Lakini, kwa nini?

"Kwa Chelsea itanizuia kuhama? Naweza kukaa hapa hadi nife! Miaka 20 au 25, lakini huwezi kujua katika soka. Ni klabu, kwa hakika kama sifanyi kazi, labda kama wakinitaka siku moja."

### ●●● Nani anajua kesho? Nilisema timu sitawahi kuzisimamia ni Arsenal na Barca...

Mashabiki wengi wa Tottenham walikasirishwa kuona Pochettino akijiunga na mpinzani kama Chelsea wakati wa majira ya joto.

90min iliripoti kuwa angekuwa na nia ya kurejea Spurs mapema mwaka huu. Lakini hakukuwa na mawasiliano kutoka kwa mwajiri wake wa zamani, ambaye alimwajiri Ange Postecoglou Juni, mwaka huu.

Chelsea hawakuwa kwenye orodha ya klabu ambazo Pochettino alisema hataweza kuziongoza, baada ya kuwaondoa Arsenal kwa uaminifu kwa Spurs na Barcelona kutokana na upinzani na Espanyol.

"Nilisema tu timu ambazo sitawahi kuzisimamia ni Arsenal na Barcelona. Ni hisia ya ajabu kurejea baada ya miaka minne," alisema.

# KONATE AKIRI ANATAKA KUICHEZEA PSG




**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa Liverpool, Ibrahima Konate, amekiri kwamba anafikiria kuhusu uwezekano wa kuichezea Klabu ya Paris Saint-Germain ya nyumbani baadaye katika maisha yake ya soka.

Konate alitumia miaka mitano katika akademi ya vijana ya Paris kabla ya kuhamia Sochaux, ambako alifanya kazi yake ya kwanza mwaka 2017 akiwa na umri wa miaka 16. Baadaye mwaka huo huo, alijiunga na RB Leipzig na kuimarisha mchezo wake kama mmoja wa mabeki wa kati vijana bora zaidi barani Ulaya.

Katika majira ya joto ya 2021, Liverpool walimsajili kwa pauni milioni 36 kumpeleka Anfield. Tangu wakati huo, amekua mmoja wa mabeki bora wa Ligi Kuu England, ingawa amekuwa akijitahidi kujiweka sawa na amekuwa akipambana na majeraha.

Katika kiwango cha kimataifa, Konate ameichezea Ufaransa mara 13 tangu alipocheza kwa mara ya kwanza mwaka 2022 na amekuwa kipenzi cha kocha Didier Deschamps. Aliingia akitokea benchi katika mchezo wa fainali ya Kombe la Dunia mwaka jana dhidi ya Argentina ambapo walifungwa kwa mikwaju ya penalti.

Kama ilivyo kwa wachezaji wengi wa Ufaransa, Konate amekuwa akihusishwa na kurejea nchini kwao kuichezea PSG. Akiwa kwenye majukumu ya kimataifa mwezi uliopita, aliulizwa ikiwa wachezaji kutoka Parc des Princes walikuwa wakimuuza kwa wazo la kuhama.

"Sitajibu kuhusu wanachofanya! Lakini hapana, ni kweli kwamba mimi ni Mparis, lakini niko Liverpool," aliiambia RMC wakati huo baada ya sare ya bao 1-1 ya Liverpool kwenye Uwanja wa Luton Town Jumapili, Konate aliulizwa na Canal Plus kama anawazia kucheza PSG siku moja.

"Kama nikisema hapana, nitakuwa nasema uongo, lakini ikiwa unauliza, ni moja ya malengo yangu? Sivyo," alisema.



# Varane awindwa Saudia

**MANCHESTER,** England

TIMU za Saudi Arabia ikiwamo Al Nassr zimeanza kuwasiliana na wawakilishi wa beki wa kati wa Manchester United, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30, ili kuipata huduma yake dirisha lijalo la majira ya baridi.

Dirisha lililopita la usajili, jina la beki huyo kutoka nchini Ufaransa lilikuwa miongoni mwa mastaa waliosakwa kukipiga Ligi Kuu ya Saudi Arabia, lakini ilishindikana baada ya Man United kugoma kumuuza.

Al Nassr inaongoza kwenye harakati za kuinasa saini yake na hasa kutokana na nyota huyo kuwa na ukaribu na nyota wa timu hiyo, Cristiano Ronaldo waliocheza pamoja kule Real Madrid.

Beki huyo inadaiwa atawekewa mshahara wa pauni 500,000 kwa wiki kama atasaini kwenye moja ya timu za Saudia.

Varane ambaye kwa sasa yupo nje ya uwanja kutokana na majeraha ana mkataba wa kuendelea kusalia Man United hadi mwaka 2025 na anaonekana kuwa mmoja kati ya wachezaji tegemeo wa 'Mashetani Wekundu' hali inayoonesha huenda akapewa ofa ya kusaini mkataba mpya.

Tangu kuanza kwa msimu huu amecheza mechi tisa za michuano yote na majeraha ndiyo yamekuwa yakiathiri soka lake pale Old Trafford.

# Aston Villa yaonywa kuhusu Emery

**LONDON,** England

KLABU ya Aston Villa imeonywa kuishi kwa akili kwa sababu Kocha wao, Unai Emery, atapewa dili kubwa na klabu inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya na hatalikataa.

Hayo ni kwa mujibu wa beki wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher, ambaye amedai kuwa anachofanya raia huyo wa Hispania kwenye kikosi hicho pale Villa Park kinampa nafasi kubwa ya kuchukuliwa na timu kubwa zaidi.

Hadi sasa kikosi hicho cha Emery kimefungwa na Manchester City, Arsenal na Liverpool na ndizo zilizoshinda alama nyingi kwenye Ligi Kuu England kuzidi Aston Villa tangu kocha huyo alipojiunga nao Novemba mwaka jana.

Carragher alidai pia kocha huyo wa zamani wa Villarreal bado ana biashara zake hajazimaliza kwenye timu kubwa baada ya kuwahi kupita kwenye timu za Paris Saint-Germain na Arsenal.

Na madai ya beki huyo wa zamani wa England tayari yatakuwa kwenye orodha ya makocha wanaosakwa na timu kubwa.

Carragher mwenye umri wa miaka 45, alisema Aston Villa wanapaswa kumshukuru Emery kwa kadri wanavyoweza na kwamba ni suala la muda tu kabla ya kocha huyo hajaletewa ofa tamu na klabu za Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambayo hataweza kuigomea.

Emery alishinda taji la Europa League mara tatu alipokuwa na kikosi cha Sevilla na mara moja akiwa na Villarreal na aliongoza PSG kushinda ubingwa wa Ligue I wakati anainoa.



## HABARI MICHEZO




# MKUDE: MAPEMA SANA YANGA KUWAZA UBINGWA

**Na Saada Akida**

KIUNGO wa Yanga, Jonas Mkude ameweka wazi kuwa licha ya kushinda mechi ya watani wa jadi dhidi ya Simba, ni mapema sana kusema tayari wameshaingia katika nafasi nzuri ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkude alisema anaamini kwa kujiandaa na kutafuta pointi tatu muhimu katika kila mechi ambayo iko mbele yao ndicho kitu pekee kitakachowawezesha kufikia malengo yanayotarajiwa na wanachama na mashabiki wa Yanga.

Alisema kitendo cha kumfunga Simba hakina maana kuwa wamemaliza kila kitu na kujihakikishia ubingwa kwa sababu ligi bado ni ndefu na wana mechezo zaidi ya 20 ambayo hawajacheza.

"Ushindi wa Simba unatuweka katika nafasi nzuri za kujihakikishia tunaendelea kusalia kileleni, suala la ubingwa ni mapema sana tunatakiwa kushinda na kutafuta matokeo chanya kila mechi ili kufikia malengo yetu na yanayotarajiwa na Wanayanga.

Ligi imekuwa na ushindani mkubwa kwa kila timu kujiandaa vizuri, tumeshinda mechi kubwa lakini unaweza kupoteza mechi ndogo, tunaamini katika kujiandaa," alisema kiungo huyo.

Aliongeza kuwa anaimani kubwa ya kufanya vizuri kwenye ligi kulingana na kila mchezaji ndani ya Yanga malengo yake ni kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo ili kutetea ubingwa msimu huu.

# KVZ FC yaivulia kofia Kipanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Wanajeshi wa Kipanga FC, Kocha wa Maafande wa KVZ FC, Ali Mohamed, amekiri uwezo mkubwa wa wapinzani wao hao katika mchezo huo wa Ligi Kuu Zanzibar uliopigwa kwenye Uwanja wa Mau A juzi.

KVZ FC ambayo katika mchezo huo ilitokea nyuma na kushinda, mabao yake yalifungwa na Kassim Hassan dakika ya 66 na Mohamed Massoud dakika ya 83 wakati William John aliwatanguliza Wanajeshi wa Kipanga FC kuliona lango la wapinzani wao dakika ya 20.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Kocha wa KVZ, Mohamed, alisema pamoja na kupata alama tatu wapinzani wao walicheza kandanda safi hasa kipindi cha kwanza ambapo waliutawala mchezo.


Alisema kipindi cha kwanza timu yake haikuwa sawa hali iliyosababisha wapinzani wao kupata bao la mapema na wachezaji wake walitoka mchezoni baada ya kufungwa. Alisema kama mwalimu kipindi cha pili alilazimika kufanya mabadiliko hasa kwa upande wa mabeki ili kuweza kuubadilisha mchezo huo na mpango wake ulifanikiwa.

"Kipindi cha kwanza hatukucheza vizuri, tulitawaliwa karibu dakika 30, lakini baada ya kurudi mapumziko nilikuja na mpango mwingine ambao ulizaa matunda na kufanikiwa kupata ushindi," alisema.

Aidha, alisema jitihada zake anaelekeza katika mchezo wa 10 dhidi ya Uhamiaji FC Jumamosi wiki, ili mchezo huo nao apate alama tatu zitakazosaidia kusonga mbele katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

KVZ FC imefikisha alama 19, huku vinara wa ligi hiyo, Maafande wa JKU wakiwa na pointi 20 na nafasi ya tatu ikishikiliwa na Maafande wa Zimamoto SC wenye alama 17.

## KUELEKEA AFCON 2027...




Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, akichangia mada katika kikao cha Mawaziri wa Michezo wa Tanzania, Kenya na Uganda pamoja na wataalamu kutoka nchi hizo kuweka mikakati ya pamoja kuelekea mashindano ya Fainali za Mataifa Afrika (AFCON) 2027 zitakazofanyika kwa ushirikiano wa nchi hizo. Kikao hicho kilifanyika Mombasa nchini Kenya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Yanga kazi moja tu Mkwakwani

INATOKA UKURASA 24

zoezini kujiandaa na mchezo wetu wa kesho (leo), utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa ila tumejiandaa vizuri na wachezaji wako tayari, tuna waheshimu wapinzani wetu licha ya kutopata matokeo mazuri katika michezo yao ya nyuma tutacheza kwa tahadhari kubwa kufikia malengo yetu," alisema kocha huyo.

Naye Kocha wa Coastal Union, Fikiri Elius, alisema wamefanyia kazi makosa yao na kikosi kipo tayari kutumia vizuri uwanja wa nyumbani kuhakikisha wanabaki na alama katika dimba la Mkwakwani.

"Licha ya Yanga kuwa bora, lakini kuna makosa wanafanya tutayatumia kutafuta matokeo mazuri ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kujiondoa chini ya msimamo," alisema Fikiri.

# Robertinho aacha timua

INATOKA UKURASA 24

huo mmoja wa Jumapili dhidi ya Yanga.

Rekodi zinaonyesha kuwa msimu uliopita aliiongoza Simba kucheza mechi 11 za Ligi Kuu bila kupoteza ikishinda mechi tisa na sare mbili.

Mechi yake ya kwanza alipojiunga ilikuwa ni dhidi ya Mbeya City, Januari 18 mwaka mwaka huu, ikiwa ni Ligi Kuu msimu uliopita Simba ikishinda mabao 3-2, Dodoma Jiji bao 1-0, Singida Big Stars 3-1, Mtibwa Sugar 3-0, Ihefu 2-0, Yanga 2-0, Ruvu Shooting 3-0, Polisi Tanzania 6-1, Coastal Union 3-0, ikitoa sare mara mbili ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC na Namungo FC.

Msimu huu imecheza mechi sita bila kupoteza ikianza kwa kuifunga Mtibwa mabao 4-2, Dodoma Jiji 2-0, Coastal Union 3-0, Prisons 3-1, Singida Fountain Gate 2-1, Ihefu 2-1, kabla ya kufungwa mabao 5-1 dhidi ya Yanga.

Mechi zingine ni za Ngao ya Jamii msimu huu, Ligi ya Mabingwa Afrika pia michuano ya African Football League dhidi ya Al Ahly ambayo walitoka sare ya mabao 2-2 Uwanja wa Benjamin Mkapa kabla ya kwenda kupata sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa wa Cairo, Misri, hivyo kutolewa kwa kanuni ya faida ya bao la ugenini.

### KUTIMULIWA

Taarifa iliyotolewa jana mchana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Imani Kajula, ilieleza kuwa wamefikia makubaliano ya pande zote mbili, huku ikimshukuru Robertinho kwa mchango mkubwa kwenye klabu hiyo.

Simba pia imemtimua Kocha wa Viungo, Hategekimana, ikisema imekubaliana naye kusitisha mkataba.

"Klabu ya Simba imefikia makubaliano ya pande zote mbili ya kuvunja mkataba na Kocha Mkuu wa kikosi cha kwanza, Roberto Oliveira Goncalves Do Carmo, 'Robertinho.

"Vilevile tumefikia makubaliano ya kusitisha mkataba wa Kocha wa Viungo, Corneille Hetegekimana. Uongozi wa Simba unawashukuru makocha hawa kwa mchango wao ndani ya klabu yetu na inawatakiwa kila la heri katika majukumu yao mapya."


# Michezo

Jumatano Novemba 8, 2023

Nipashe




Pochettino afungua mlango kurejea Spurs UKURASA 21




# ROBERTINHO AACHA TIMUA TIMUA SIMBA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## Sven atajwa kumrithi, mastaa watano waingia kikaangoni, Mangungu, Try Again nao...

SIKU mbili tu baada ya kupata kipigo cha fedheha cha mabao 5-1 kutoka kwa watani zao wa jadi, Yanga, Klabu ya Simba imeamua kuachana na kocha wake mkuu, Robertinho Oliveira, raia wa Brazil sambamba na Kocha wa Viungo, Corneille Hategekimana, huku 'moto wa timuatimua' ukiendelea kuwaka Msimbazi.

**Kwa mujibu wa taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili ni kwamba, licha Robertinho 'kuangukiwa na jumba bovu', lakini ndani ya Simba bado moto unawaka baada ya Mwekezaji na Rais wa Heshima wa timu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, kutofurahishwa na mwenendo wa timu hiyo huku akitaka viongozi kujitathmini.**

Viongozi hao ni Mwenyekiti wa Wanachama, Murtaza Mangungu na wa Bodi ya Wakurugenzi, Salim Abdallah 'Try Again, ambao inadaiwa wametakiwa kujiuzuru kutokana na kitendo cha timu hiyo kupoteza mchezo dhidi ya watani wao wa jadi.

Mtoa habari huyo alisema moto huo hautakuwa kwa viongozi hao pekee bali utashuka kwa baadhi ya wachezaji ambao nao watakuwa wamekalia kaa la moto wakitakiwa kutoa maelezo.

"Robertinho ametolewa 'kafara' tu, lakini ndani ya uongozi kuna mambo mengi, viongozi wametakiwa kujitathmini hasa kuanzia usajili wa baadhi ya wachezaji, lakini pia kuhujumu timu na kupoteza mbele ya mtani wetu, Yanga kwa mabao 5-1.

Pia, kutokuwa na maelewano mazuri na wajumbe 21 walioteuliwa na tajiri huyo kwa ajili ya kumshauri kuhusu klabu ambao waliwahi kupita Simba katika ngazi mbalimbali," alisema mtoa habari huyo.

Aliongeza kuwa tangu imeteuliwa kamati hiyo, haijawahi kukutana na Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba kuzungumza lolote, wala kupewa barua rasmi ya uteuzi huo, na kwamba hiyo ni kutokana na mgongano wa kimaslahi.

Alisema Mo Dewji kwa sasa yupo Dubai na anatarajia atakaporejea nchini kuanza mchakato wa haraka kutafuta kocha mkuu ambaye atakuja kuchukuwa mikoba ya Robertinho, huku Kocha wao wa zamani, Mbelgiji Sven Vandenbroeck akitajwa.

Sven kwa sasa hana timu baada ya mwezi uliopita kufutwa kazi na Klabu ya CR Belouizdad ya Algeria kutokana na matokeo mabovu kwenye Ligi Kuu.

### REKODI YA ROBERTINHO

Hata hivyo, Robertinho ambaye ameondolewa kwenye klabu hiyo baada ya kuhudumu kwa miezi 10 tu, ameacha rekodi ya kuvutia ambayo inawagusa mashabiki wengi wa klabu hiyo.

Mbrazili huyo ameiongoza Simba mechi 29 za mashindano yote huku akipoteza mbili tu, moja Ligi ya Mabingwa msimu uliopita dhidi ya Wydad Casablanca baada ya kushinda 1-0 nyumbani na kwenda kupoteza 1-0 ugenini.

Nyingine ni ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga Jumapili iliyopita, lakini akiipa Simba Ngao ya Jamii kwa kuifunga timu hiyo kwa mikwaju ya penalti 3-1.

Kocha huyo aliifikisha Simba kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya robo fainali na kuondoshwa na waliokuwa mabingwa watetezi wakati huo, Wydad Casablanca ya Morocco kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Ameiongoza Simba katika mechi 18 za Ligi Kuu, tangu msimu uliopita, ikishinda michezo 15 na sare mbili tu na kupoteza

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yataka kazi moja leo Mkwakwani

**Na Saada Akida**

KITUO kinachofuata ni Mkwakwani, Tanga! Hii ni kauli ya Wanayanga wakisema kuwa wanakwenda jijini humo kuendeleza zoezi la kutoa dozi na kusaka pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya wenyeji wao, Coastal Union leo.

Kikosi cha Yanga kimewasili tangu juzi usiku jijini Tanga tayari kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu katika mchezo huo ili kuendelea kujiimarisha kukaa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

Yanga inashuka dimbani na kumbukumbu nzuri ya kupata ushindi mnono wa mabao 5-1 katika mechi kubwa dhidi ya watani wao wa jadi, Simba na kukaa kileleni ikiwa na alama 21.

Coastal Union wenyewe walitoka suluhu katika mchezo uliopita dhidi ya Namungo FC katika dimba hilo la Mkwakwani, wakiwa nafasi ya 13 baada ya kukusanya alama saba katika michezo nane waliyocheza ya ligi hiyo hadi sasa.

Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema baada ya mechi ya 'dabi' dhidi ya Simba, waliendelea na maandalizi kujiandaa na mechi ya leo dhidi ya Coastal Union.

Alisema walifanya mazoezi ya gym na baadaye kujiweka sawa na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mchezo huo kutafuta alama tatu muhimu ili kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo.

"Hatukuwa na muda baada ya mechi kubwa, tukarudi ma-



INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >